# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 19, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0581681

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Watimuliwa** kwa madai ya kuhamasisha vitendo ushoga

UKURASA 2

**Mtoto** miaka 10 adaiwa kubakwa, polisi washikwa na kigugumizi

UKURASA 5



**Serikali** yajipanga kudhibiti uhaba wa mafuta ya kupikia

UKURASA 8



**Bambo amng'ang'ania Diamond**

UKURASA 20

# Maswali magumu Askofu kujinyonga

• **Viongozi** wa dini watoa kauli nzito... *Endelea ukurasa 2*



"Kiongozi huyo amekengeuka kiimani kutokana na kitendo cha kujiua, ukizingatia kuwa maandiko yanakataza kujinyonga tena wanaofanya hivyo mbinguni hawataingia." – **Askofu Anthony Mlyashimba**



"Kama ni madeni hata serikali inadaiwa. Iweje yeye aamue kujinyonga kwa kuhofia madeni hayo?"- **Sheikh Rajab**



"Ni vigumu kuamini lakini imetokea. Jambo hilo ni geni kwa Askofu kujinyonga na limeliweka kanisa katika njia panda." – **Mch . Dk. Mlyuka**

## Nesi asimulia walivyompokea Lissu baada ya kupigwa risasi

UKURASA 3



# Hivi ndivyo ilivyo hatari ya kutokuandika wosia

• **Milioni** 430/- zakosa warithi, zapelekwa BoT... *Endelea ukurasa 4*

**Na Jaji Ilvin Mugeta,** ARUSHA

KIFO ni jambo la uhakika kwa kila kiumbe chenye uhai. Sayansi na vitabu vya dini vimethibitisha. Baada ya kifo, nyuma hubaki mali zinazopaswa kurithiwa.

Hata hivyo, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2003 hadi 2008, zaidi ya Sh. milioni 430/- zilikosa warithi wa wanahisa wa Benki ya CRDB. Zikapelekwa Benki Kuu (BoT). Hii ni hasara ...



**MICHEZO** YANGA, IHEFU MECHI YA KISASI UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kimpungua, Manispaa ya Singida wakisoma darasani huku wakiwa wamekaa chini ya sakafu shuleni hapo, juzi. Shule hiyo, yenye jumla wanafunzi 1,182 inakabiliwa na upungufu wa madawati 162, uliosababisha wanafunzi zaidi ya 486 kukaa chini. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Maswali magumu Askofu kujinyonga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KIFO cha Askofu Mkuu wa Kanisa la Methodist Tanzania, Joseph Bundala, kilichotokana na kujinyonga kimeibua maswali magumu na mshangao kwa jamii kutokana na kitendo hicho kuwa kigeni ndani ya jamii.

Wakati maswali hayo yakionekana kukosa majibu, baadhi ya viongozi wa dini wameibuka na kulaani kitendo hicho kuwa ni kinyume cha maandiko matakatifu, hususan katika ukristo.

Kutokana na nafasi ya kiongozi huyo wa kanisa kuchukua uamuzi huo, miongoni mwa maswali ni je, maziko yake yatakuwa katika itifaki na utaratibu wa Kikristo? Hiyo inatokana na hali iliyozoeleka kwamba Mkristo akijiua au kujinyonga anazikwa bila ibada, hivyo swali linaibuka kama ibada na itifaki za maziko kwa kiongozi wa dini zitafanyika.

Askofu au mchungaji katika madhehebu ya Kikristo anapofariki dunia, maziko yake hufanyika kwa ibada maalum ambayo hujumuisha maaskofu au wachungaji kulingana na wadhifa au hadhi yake. Ibada hiyo pia huendana na maaskofu au wachungaji kusoma maneno kutoka katika Biblia Takatifu.

Swali lingine ni kwa nini achukue hatua kama hiyo kwa sababu alizozitaja ilhali kwa nafasi yake amekuwa akikutana na watu wenye matatizo na migogoro na kuisuluhisha.

Aidha, akiwa Askofu Mkuu ina maana kwamba chini yake kuna maaskofu katika maeneo mengine ambao angeweza kuwashirikisha na kumsaidia kuondokana na matatizo yaliyokuwa yakimkabili nani kwa nini hakufanya hivyo mpaka kuamua kujiua kwa kujinyonga.

**VIONGOZI WA DINI**

Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecoste Holiness Association Mission Tanzania, Askofu Julius Bundala, akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo jana jijini hapa, alisema kitendo cha kiongozi huyo wa dini kujinyonga, kimeidhalilisha dini, serikali na jamii kwa ujumla.

Askofu Bundala alisema kiongozi huyo alikuwa akiaminiwa na kanisa, waumini na serikali, hivyo kitendo cha kujinyonga kwake hakikubaliki kwa kiongozi mkubwa kama yeye.

"Pia hata kwa kanisa lake ambalo alikuwa akiliongoza, waumini watakuwa na mashaka. Hata viongozi wengine waliobaki na pia itakuwa vigumu kushawishi kwa watu wengi wenye kutaka kujinyonga kuwashauri wasifanye hivyo," alisisitiza.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Jacol Memeo Ole Paulo, alisema suala hilo halijazoeleka kwa viongozi wa dini kuchukua uamuzi wa kujiua au kujinyonga.

Hata hivyo, alisema viongozi wa dini ni binadamu na si malaika, hivyo wasiposimama katika maombi na kujikita katika neno la Mungu, ni rahisi kuingia katika majaribu na hata kuchukua uamuzi kama huo.

"Maaskofu na wachungaji wana kazi kubwa na wanakutana na mengi. Jambo la muhimu ni kusimama katika imani na kumwomba Mungu tu ili akushindie," alisema.

Mchungaji wa KKKT na mwanataaluma, Dk. Enock Mlyuka, alisema kitendo hicho cha Askofu kuchukua uamuzi wa kujinyonga na kukatisha uhai, kimeishtua jamii na kanisa kwa ujumla.

"Ni vigumu kuamini lakini imetokea. Katika kanisa jambo hilo ni geni kwa Askofu kujinyonga. Kwa kweli jambo hili limeliweka kanisa katika njia panda," alisema.

Naye Mwenyekiti wa viongozi wa dini na madhehebu ya mkoa wa Dodoma na Kamati ya Amani, Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, alisema kujinyonga si haki kwa mwanadamu yoyote.

"Kitendo alichokifanya Askofu huyo ni sawa na kujiua mwenyewe na Mungu hahusiki na kifo hicho," alisema.

Sheikh Rajabu alisema kuwa uamuzi aliouchukua kuna hatari ya kulisambaratisha kanisa pamoja na waumini kwa kuwa watakosa imani na viongozi wao hata kama watakuwa wakihubiri ubaya wa kujinyonga.

"Kama ni madeni hata serikali inadaiwa. Iweje yeye aamue kujinyonga kwa kuhofia madeni hayo. Mimi kama kiongozi kitendo alichokifanya si mpango wa Mungu bali ni shetani alimzidi kete," alisema Sheikh Rajabu.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoa wa Dodoma, Askofu Anthony Mlyashimba, alisema kiongozi huyo amekengeuka kiimani kutokana na kitendo cha kujiua mwenyewe.

"Ukizingatia kuwa maandiko yanakataza kujinyonga tena wanaofanya hivyo mbinguni hawataingia," alisema.

Askofu Mlyashimba alisema kuwa kiongozi huyo alikuwa akitegemewa na kanisa, familia pamoja na serikali. Ni imani yake kwa viongozi wengine waliobaki wataendelea kuhubiri matendo mema ikiwa ni pamoja na kukataza hatua za kujidhuru na ubaya wa ukatili.

Askofu Mkuu Bundala (55), alikutwa amejinyonga kwa kamba ndani ya ofisi yake iliyoko kwenye kanisani hilo, Mtaa wa Meriwa, jijini hapa huku akiacha waraka mrefu ukieleza sababu za kuchukua uamuzi huo kuwa ni madeni na mgogoro ulioko katika uendeshaji wa shule binafsi.

Bundala ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kanisa hilo kwa Afrika, mwili wake uligundulika Alhamisi saa 1:00 usiku ukiwa unaning'inia ofisini kwake.

## Watimuliwa, madai kuhamasisha ushoga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, amesema hadi sasa watu 64 wa mataifa mbalimbali na jumuiya zilizokuwa na viashiria vya mmomonyoko wa maadili, ikiwamo ushoga wametimuliwa na kufungiwa kuingia nchini.

Aidha, wakimbizi 41 wamewekewa zuio la kuingia nchini kutokana na kuhamasisha vitendo hivyo.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema hayo bungeni juzi wakati akichangia na kujibu hoja zilizotolewa na wabunge wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka 2024/25.

Katika mjadala huo, wabunge walitaka mkakati wa serikali kudhibiti vitendo vya ushoga, ulawiti na ubakaji.

Akijibu hoja za wabunge, Masauni alisema serikali haipo kimya katika kupambana na vitendo hivyo na imeendelea na vita ya kisayansi kukabiliana navyo.

"Waheshimiwa Wabunge wameonyesha uchungu katika eneo la mapambano dhidi ya ushoga, na vita dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia , nakiri kwamba vita hii ni pana sana, ni kubwa na mapambano dhidi ya vita hii ni lazima tushikamane kama nchi ili tuweze kushinda,"alisema.

Alifafanua kuwa Jeshi la Polisi linapambana kupitia sheria dhidi ya uhalifu huo ambao umeidhinishwa katika sheria zilizopo nchini ni kuwa kubaka, kulawiti, shambulio la aibu, kuzini, kumpa mimba mwanafunzi ni uvunjaji sheria namba 12 ya marekebisho ya mwaka 2022.

Alisema makosa ya ushoga, ipo kwenye sheria ya makosa ya maadili ya jamii hivyo kimsingi kupitia sheria hizo kuna mambo yamefanyika ikiwemo kuwachukulia watu wanaofanya hivyo hatua kwa kuwaondoa nchini ambao wanaleta habari ambazo hazipo katika misingi ya mila, sheria na utamaduni wa kitanzania.

Kuhusu adhabu na dhamana, alisema ni masuala ya kisheria na kwamba bunge ndio lina mamlaka ya kufanya mabadiliko hivyo serikali imepokea hoja hiyo ya msingi watakaa pamoja kutafakari kama kuna haja ya kuangalia sheria hizo ili zifanyiwe maboresho.

Kwac upande wa Idara ya Uhamiaji, alisema ana orodha wa watu 64 ambao wametimuliwa nchini na kuwapiga marufuku kuingia nchini kutoka mataifa mbalimbali waliogundulika kwamba wana viashiria vya ushoga.

"Pia wako wakimbizi 41 wamepigwa Prohibited Immigrant (kuzuiwa mipakani wasiingie nchini) ni marufuku kuingia katika nchi hii, kwahiyo kazi hii inaendelea, taasisi vilevile jumuiya zinazosajiliwa kuna ambazo zimefungiwa hivyo kuna hatua ambazo zinachukuliwa na kila sehemu katika kupambana na vita hii,"alisema.

HABARI KITAIFA

# Muuguzi asimulia alivyompokea Lissu aliposhambuliwa kwa risasi

**Na Romana Mallya**

MUUGUZI aliyemhudumia Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokraasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, baada ya shambulio la risasi, amesimulia walivyompokea, huduma waliyompatia na neno lake la mwisho kabla ya kuzirai.

Akisimulia mkasa huo kupitia video iliyosambaa mtandaoni baada ya Lissu kukutana na muuguzi huyo aliyejitambulisha kwa jina la Veronica, alisema wakati anafikishwa hospitalini hapo, yeye na wenzake akiwamo daktari aliyemtaja kwa jina la Bundala, walikuwa Idara ya Wagonjwa wa Nje (OPD).

"Tulikupokea OPD ukiwa umeloa damu, huyu baba alikuwa ameloa damu kutoka mwilini kwako, tukakuingiza chumba cha dharura. Ninataka nikupe sentensi yako ya mwisho uliyoongea na mimi. Huwezi ukanikumbuka. Kiukweli mheshimiwa uliumia.

"Sasa tulikuwa tukishika mkono unaning'inia. Tukikamata huku unaning'inia, tukishika mguu unaning'inia. Tukawa tunaendelea kukuhudumia ili damu isiendelee kutoka lakini ikawa inatoka.

"Ikabidi tuchukue toroli. Nilikuwa mimi na nesi anayeitwa Elizabert, Daktari Bundala, tukakimbia mpaka chumba cha upasuaji. Kufika bahati mbaya tukakuta madaktari wamemaliza upasuaji wametawanyika," alisimulia.

Muuguzi huyo alisema kutokana na hali hiyo, ilibidi yeye na wenzake waendelee kumhudumia wakati madaktari wakitafutwa huku daktari Samwel akiwa wa kwanza kuingia wakimsubiri mwingine.

"Tukikuangalia tunaona unaendelea kutokwa damu ndipo nilipochana bukta yako," anasimulia nesi huyo huku Lissu akimtania alikuwa amevaa bukta au suruali na kumweleza kuwa suruali waliitupa OPD na anaongea hayo kwa kuwa anaona sasa anapumua.

"Huyu baba aliumia. Sisi hatukuwa wasemaji lakini mimi ndiye muuguzi niliyempokea na hata dereva ndiye niliyemkabidhi zile nguo, Mheshimiwa (Freeman) Mbowe (akiwa) pembeni. Nilifika na nguo zake nikitokea chumba cha upasuaji. "Ila kabla sijatoka (chumba cha upasuaji) ulianza kutoka jasho, huku daktari anakutundikia dripu mkono mwingine, ulichotamka ulisema, "Please Doctor do something for me" ukalegea.

"Nilitoka na damu, mtu wa maabara alikimbia, kupima ulikuwa na damu tatu. Ninaongea ukweli mbele za Mwenyezi Mungu, huyu Mheshimiwa damu ilikuwa tatu. Kilichoendelea ninafikiri unajua," alimweleza Lissu huku akijibu, atajuaje.

Alisema akiwa muuguzi, aliishia hapo na kukabidhi nguo na kwenda kuchukua damu wakati madaktari wakiendelea na upasuaji wake.

"Ulichotamka ni 'Doctor do something for me', uliongea Kiingereza hukuongea Kinyaturu," alimsimulia, huku Lissu akimpa pole akimweleza wanaona vitu vya ajabu.

"Mimi sikuviona vyote hivyo," alisema Lissu huku muuguzi huyo akimtaka amshukuru Mungu wake mpaka sasa yupo.

Alimweleza kuwa wanapofanya kazi alafu mgonjwa akapona wanapata baraka na kushukuru na kwa hali yake, hakutegemea siku moja angekutana naye.

Baada ya maelezo hayo, Lissu alihoji kwa nini wanajificha wakati madaktari wake wote na manesi waliomtibu Nairobi, Kenya anawafahamu lakini hapa huyo ndiyo wa kwanza anakutana naye.

Muuguzi huyo alimfafanulia kwamba taratibu za Tanzania ni tofauti ndiyo maana hata siku ya tukio walipokuwa wakipiga picha, kiongozi wao aliwataka wakae pembeni wasionekane.

"Unajua pale hospitalini palijaa watu, tukawa tunaogopa usalama wako. Hakuna mtu aliyeruhusiwa kuingia chumba cha upasuaji bila kitambulisho na tulifunga milango yote, sisi wa mapokezi tukarudi kuendelea na kazi zetu, huku tukipata taarifa unavyoendelea mpaka ulipokwenda Nairobi.

"Ila chupa za damu baba ulikula. Madaktari waliokuhudumia walikuwa ni Dk. Samwel na Dk. Ibenus ndiyo waliokuwapo pale," alisema.

Muuguzi huyo alimweleza Lisu kuwa alipoteza fahamu pale alipokuwa akimtundikia dripu na kutamka sentensi yake ya mwisho. Muuguzi huyo alisema kwa sasa ana miaka miwili hayupo kazini, aliondoka Aprili, 2020.

**MJADALA UNUNUZI GARI**

Katika hatua nyingine, siku moja baada ya Jeshi la Polisi kumkabidhi gari lake Lissu, mjadala umeibuka mtandaoni huku baadhi wakitaka kumchangia fedha ili kununua jipya, wengine wakiona hoja hiyo ni mzaha kwao.

Manaharakati Maria Sarungi, katika ukurasa wake wa Instagram juzi baada ya Lissu kukabidhiwa gari lake lililokaa polisi kwa miaka saba, aliibua hoja ya kumchangia fedha ili anunue gari jipya.

Sarungi aliweka tangazo lenye maelezo yanayosomweka: "Tumchangie Tundu Lissu anunue gari jipya," huku akiweka namba za kupokelea na akaunti.

Aliwataka wale wanaotaka gari la Lissu liwekwe kumbukumbu wazingatie kwamba hana gari kwa sasa, anakodi kwa fedha nyingi na hawezi kumudu. Pia alisema Lissu anahitaji gari ili kuzunguka nchi nzima kutoa elimu.

Baadhi walipokea hoja hiyo na kupendekeza anunuliwe gari aina ya Land Cruiser 300 (LC300) huku wengine wakiona ni kichekesho kumnunulia mtu mwenye fedha gari wakati familia zao hazina chakula.

Wakati mjadala huo ukiwagawa wachangiaji, mwingine amependekeza gari alilokabidhiwa na polisi lisiguswe liachwe lilivyo kwa kuwa litaacha alama kubwa na kueleza kuwa ifikapo Mei 30, atakuwa na gari lingine.

Mchangiaji anayejiita bin.rama, alichangia kwa kuweka emoji ya kucheka na kuandika: "Mbona uhuni wa macho macho unatuletea wewe bi mkubwa. Ok (sawa) toka lini magari wanayozunguka nayo CHADEMA wanakodisha? Maruzuku wanayopewa unaweza kuniambia kazi yake nini?"


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende "pay via mobile". Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Jaji: Hii ndiyo hatari ya kutoandika wosia

## ●Milioni 430/- zakosa warithi wa wanahisa CRDB, zapelekwa BoT, ni hasara kwa marehemu, wapendwa wao

JAJI wa Mahakama Kuu - Iringa, Ilvin Mugeta ameonya kuwa ni hatari kutoandika wosia, akishauri kila mwenye mali kuandika ili kuwalinda warithi wake.

Jaji Mugeta alitoa angalizo hilo juzi alipowasilisha mada juu ya Wosia na Mirathi wakati wa semina ya uwekezaji na elimu ya fedha iliyoandaliwa na Benki ya CRDB kwa wanahisa wake na Watanzania kuelekea Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa benki hiyo uliofanyika jana katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), jijini Arusha. Ifuatayo ni sehemu ya wasilisho hilo:

Kifo ni jambo la uhakika kwa kila kiumbe chenye uhai. Sayansi na vitabu vya dini vimethibitisha. Biblia katika kitabu cha Mwanzo 3:19 inasema, "kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi." Quran katika Surat Imran 3:185 inasema, "kila nafsi itaonja umauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya kiama."

Baada ya KIFO, nyuma hubaki MALI zinazopaswa kurithiwa. Magonjwa, uzee, ajali na vyanzo vingine vya kifo vimempa mwanadamu uhakika, ufahamu na uzoefu mkubwa wa uwapo wa kifo. Vimethibitisha kuwa:

Kuna alama za kifo: Vyumba vya kuhifadhi maiti, makaburi ya umma na majumbani. Vyote vinamkumbusha mwanadamu hai ajiandae kimwili na kiroho!

Muda wa kufa haujulikani lakini utafika. Pengine umekaribia kufika au bado uko mbali (miaka 70) ambapo wengi hawafiki.

### MAANDALIZI

Kiroho - maisha baada ya kifo (peponi na jehanamu). Kwa wanaoamini kiama. Kimwili - mali zake zitakavyotumika au kugawanywa baada ya kifo (uhusiano wa kifo na mali). Baada ya kifo ungependa mali zako zitumikeje?

Weka utaratibu wa kufuatwa kwa ajili hiyo baada ya kifo chako. Changamoto iliyopo ni kwamba wenye afya wanadhani kuwazia kifo ni jukumu la walio katika hatari ya kifo.

### SABABU KUTOJIANDAA

Sababu za kutowaza juu ya kifo ni nyingi. Mathew Hale, Jaji Mkuu wa Uingereza (1609-1976) anaeleza sababu tatu: Kifo ni jambo lisilokubalika. Kuwaza juu ya kifo kunasababisha usiifurahie leo yako; kuwaza na kupanga juu ya kifo ni uchuro. Ajabu ni kwamba hata wasiowaza hufa; na ni mzima sasa, kwanini uwaze juu ya uwezekano wa kuumwa au kufa kesho? Mawazo ya kifo ni kwa wazee.

Ukweli wa mambo ni kwamba, kutojiandaa ni upuuzi. Kutafakari juu ya kifo ni faida: Unajifunza kuishi vyema katika jamii na utaandaa WOSIA bila kuchelewa na mali zako hazitapotea.

### MADHARA KUTOJIANDAA

Kuna madhara makubwa usipojiandaa. Ushahidi ni mali zilizopotea. Takwimu za gawio zilizokosa wa kuzirithi katika benki ya CRDB.



Jaji wa Mahakama Kuu Iringa, Ilvin Mugeta

| Mwaka | Idadi wanahisa | Fedha (Sh.) |
|---|---|---|
| 2003 | 2,492 | 36,882,223 |
| 2004 | 2,269 | 41,346,760 |
| 2005 | 1,464 | 50,224,725 |
| 2006 | 2,427 | 61,990,262 |
| 2007 | 2,129 | 94,453,051 |
| 2008 | 5,891 | 146,459,062 |

Hii ina maana kwamba jumla ya Sh. milioni 431.296 zimekosa warithi baada ya wanahisa wa CRDB kufariki dunia, hivyo kupelekwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa mujibu wa sheria kutokana na wanahisa hao kutoandika WOSIA.

### TAKWIMU KORTINI

Takwimu za mahakamani zinaonesha ni asilimia tatu pekee ya kesi mahakamani ndizo zina wosia: Asilimia 80 ya kesi Mahakama Kuu hazina wosia; asilimia 90 ya kesi mahakama za wilaya hakuna wosia na asilimia 99.9 ya kesi katika mahakama za mwanzo hakuna wosia.

Takwimu hizi ni kiashiria cha kutojali: Mwislamu mwenye mtoto nje ya ndoa zingatia mirathi isizidi theluthi moja ya mali yote. Mkristo mwenye mtoto nje ya ndoa zingatia pia.

### VISA MAHAKAMANI

Kuna mifano halisi ya visa mahakamani: Watoto ambao hivi sasa ni watu wazima wanataka nyumba ya baba iuzwe wagawane na mke wa marehemu; mke na watoto wameuawa ili ndugu warithi mali; watoto wa kike wamenyimwa urithi kwa kuzingatia mila za marehemu: na dada anasimamia mirathi, anauza mali na kula. Nyaraka za kufungulia kesi ameghushi na wadhamini wanakana kutia saini nyaraka za kufungulia kesi.

Ushauri wangu: Epusha usumbufu kwa wapendwa wako kwa kuandika wosia. Mafao si sehemu ya mirathi - weka kumbukumbu zako sawa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

### MIRATHI

Ni mchakato wa kisheria wa kusimamia mali za marehemu ziweze kuwafikia warithi wake. Mirathi ipo ya aina mbili ambazo ni mirathi ya wosia na mirathi isiyokuwa na wosia. Sheria inayohusika katika mirathi ya mtu ndiyo huamua.

Wosia ni maandishi aliyoacha marehemu, akieleza: Mali zake, mtu wa kusimamia atakapofariki dunia (mtekeleza wosia), orodha ya warithi wake na mgawanyo wa mali hizo kwa warithi.

Kwa kuacha wosia, mwenye mali anakuwa na hakika utashi wake utasimamiwa, mali zake zitatambulika na kuwafikia warithi bila upotevu (fedha za gawio). Mali zikikosa warithi zinakuwa mali ya serikali.

### MIRATHI YA WOSIA

Taratibu za kufungua mirathi yenye wosia ni rahisi kwa vile wosia unataja msimamizi. Mahakamani hoja ni kuthibitisha tu kama kweli wosia uliandikwa kwa viapo vya wale walioshuhudia wosia.

Hakuna haja ya vikao vya wanandugu kuteua mtu anayekubalika kwa warithi wote.

### HUDHIBITI WENYE TAMAA

Ugawaji umerahishwa kwani marehemu mwenyewe ndiye amegawa. Wafahamishe warithi juu ya kuwapo wosia bila kuwaeleza kilichomo.

### MIRATHI BILA WOSIA

Marehemu haachi maandishi juu ya mali zake na matumizi yake. Hivyo: Utambuzi wa mali za marehemu hutegemea taarifa za watu wake wa karibu; mizozo huzuka miongoni mwa wenye sifa za kusimamia mirathi, msimamizi wa mirathi anaweza kugawa mali kinyume cha ambavyo marehemu angependa iwe. Wakishachaguliwa mamlaka yao ni makubwa sana (Bhakome), na hasara kwa uwezekano wa baadhi ya mali kutotambulika ni mkubwa. Dhuluma kwa wajane/ watoto wa kike na wenye ulemavu.

Hakuna uwezekano wa mtu kufikia mali za marehemu bila kufungua mirathi ma kuchaguliwa msimamizi au mtekelezaji wosia.

### CHANGAMOTO

Kuchelewa sana kufunguliwa kwa mirathi, wanafamilia kutokuwa na taarifa kuwa marehemu alikuwa na hisa, ndugu kutokubaliana nani awe msimamizi wa mirathi na wasimamizi kutofanya majukumu yao kwa moyo na kwa uaminifu. Kuepuka haya, chagua mtu unayemwamini kwa kuandika wosia.

### MAPENDEKEZO

Kila mtu anayemiliki mali anapaswa kuandika wosia ili kuwalinda warithi.

Wadau wa sekta ya benki washirikiane na mahakama na Ofisi ya Kabidhi Wasii kutoa elimu kwa umma kuhusu wosia, taratibu na faida zake.

Jielimishe kuhusu taratibu za mirathi na uliyepata elimu hii, chukua hatua sasa na mfahamishe na mwenzako. Mali tunazochuma hatuzikwi nazo baada ya kifo.

Mwenye mali akifa bila kuweka utaratibu wa upatikanaji na matumizi ya mali zake zinaweza kupotea au kutumika kinyume cha ambavyo angependa yeye zitumike.

Kuandika wosia ni hekima na ustaarabu kwani siku ya kifo haifahamiki. Wosia huepusha mafarakano katika familia. Kutoandika wosia ni hasara kwa marehemu na kwa wapendwa wake.

HABARI KITAIFA

UKATILI WA KUTISHA

# Mtoto adaiwa kubakwa na kunyongwa

**Na Romana Mallya**




Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masuni



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo

SAKATA la kijana anayedaiwa kubaka kisha kuua limesababisha mtikisiko katika vijiji vya Mianzi na Mipera, Kisarawe mkoani Pwani, baada ya mtuhumiwa ambaye hajatiwa nguvuni hadi sasa, kuonekana usiku wa manane na kutishia kwa panga wanakijiji na viongozi.

Tukio hilo ni mithili ya sinema lililoanzia nyumbani kwa mtoto huyo aliyekuwa akiishi na babu na bibi yake, likimhusisha mtuhumiwa huyo ambaye ni ndugu na marehemu.

Mtuhumiwa huyo, Ismail Mandanga, anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 26, mkazi wa Kitongoji cha Mwomboni, kijiji cha Mianzi, anadaiwa kufanya ukatili huo Jumamosi iliyopita kwa kumbaka, kumnajisi mtoto wa kike wa miaka 10 (jina hifadhiwa) ambaye ni ndugu yake, mkazi wa kijiji cha Mipera, kata ya Marui, kisha kumnyonga porini.

Wakati taharuki hiyo ikichukua siku nane sasa, kunalalamikiwa kuwapo ukimya mkubwa wa polisi kuingilia kati, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, akiiambia Nipashe kwamba tukio hilo bado halijamfikia mezani.

Mwandishi wa habari hii alipomtafuta Kamanda Lutumo kuzungumzia tukio hilo alisema: "Ngoja nifuatilie. Umesema limetokea maeneo ya Kisarawe? Ngoja nifuatilie na niweke mkazo."

**BABU AFUNGUKA**

Babu wa mtoto huyo (marehemu), Said Mwinyimkuu, ambaye alikuwa akikaa naye, anasimulia mkasa huo akisema siku ya tukio, yeye na mke wake walikuwa wamekwenda shambani, ndipo mtuhumiwa akafika nyumbani kwake na kumchukua mjukuu.

Anasimulia kuwa kijana huyo baada ya kufika nyumbani kwake, aliwakuta wajukuu zake wanne, kati yao wawili ni wenye miaka 10, akiwamo marehemu na wengine wadogo.

Baada ya mtuhumiwa kuambiwa babu na bibi wamekwenda shambani, anasema akamtaka mjukuu wake (marehemu) waongozane kwenda shambani.

"Njiani ndiyo akamvutia porini na kumfanyia ukatili huo. Baada ya hapo, Ismail akaja shambani wakati huo mimi nilikuwa nimeshaondoka, akamkuta bibi. Baadaye wakaondoka na bibi hadi nyumbani. Bibi akabaini mjukuu wake mmoja hamwoni na alipouliza, mtuhumiwa akajibu haraka, yuko msalani anajisaidia.

"Lakini bibi baada kuona muda unakwenda, mjukuu hatoki, akabaini hata huko hayupo. Aliuliza tena ndipo wajukuu wangu wakamwambia bibi yao kuwa aliondoka na kaka (mtuhumiwa) kuwafuata shambani. Mtuhumiwa ambaye wakati huo alikuwa akiongea na mjomba wake, baada ya kusikia hivyo akaondoka nyumbani kwangu na kwenda kusikojulikana," anasimulia.

**MWENYEKITI ASIMULIA**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mipera, Mwishehe Muswa, anasema eneo ambako kumetokea tukio hilo ni umbali wa urefu wa viwanja vitano vya mpira kutoka nyumbani kwa babu yake.

"Mtuhumiwa Ismail anakadiriwa kuwa na miaka 26. Mtuhumiwa na huyu mtoto aliyefariki dunia ni ndugu, mtoto wa mjomba na wa shangazi. Sehemu alikofanya tukio hilo kutoka barabarani ni umbali wa mita 50. Amembana, amemnajisi kisha kumnyonga," anasimulia.

Mwenyekiti huyo anasema baada ya wajukuu wa bibi huyo kueleza kuwa mwenzao aliondoka na mtuhumiwa, ndipo kijana huyo akawazuga kama anaingia chooni na mwishoWe kuruka ukuta na kutokomea.

"Aina ya uondokaji wake ukampa shaka bibi, machale yakamcheza na kubaini kuna kitu kimetendeka. Bahati nzuri huyu mtuhumiwa tabia zake zinajulikana kwa sababu haya matukio anayo muda mrefu, wasiwasi ukamwingia ndipo akajulisha watu," anasema.

Anasimulia kuwa wakati wanamtafuta mtoto ndipo mama mmoja akaeleza alisikia kelele ya mtoto sehemu moja kichakani, lakini hakuzitilia maanani akidhani ni watoto wanavua samaki.

Anasema baada ya kufika eneo hilo walipoingia katika pori ndipo walipokuta mwili wake chini na uchunguzi umebaini amefanyiwa ukatili huo. Anasema mwili huo ulionekana siku hiyo ya tukio na baada ya uchunguzi saa sita usiku polisi uliukabidhi kwa ndugu na kuzikwa Jumapili iliyopita.

Anasema kijana huyo ni mwenyeji wa kijiji jirani na usiku wa kuamkia Alhamis walipata taarifa ameonekana zaidi ya mara mbili (usiku na mchana) kijijini kwao Mianzi, akitishia wananchi na viongozi wa kijiji.

Mwenyekiti huyo anasema tukio hilo limezua taharuki na sasa baadhi ya wazazi wanawahamishia Dar es Salaam watoto wao baada ya kusikia mtuhumiwa anarudi usiku kutishia wananchi.

"Mpaka sasa kwenye shule yangu ya Msingi Malui Mipera leo (jana) alikokuwa akisoma marehemu, tumepanga kufanya kikao. Nimetaarifiwa kuna tatizo hili la watoto kutofika shule. Baada ya kikao tutajua ni watoto wangapi hawaonekani shule," anasema.

**MWENYEKITI ATISHIWA**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mwomboni, Ismail Muhanuka, ambako mtuhumiwa anaishi, anasema baada ya mauaji hayo, kijana huyo ameanza kutishia wananchi akiwamo yeye.

"Mtuhumiwa alikuja nyumbani kwangu Jumatano kuamkia Alhamis na Alhamisi kuamkia Ijumaa, amekuja mara mbili. Siku ya kwanza alikesha kuanzia saa 2:00 usiku hadi saa 9:00 usiku. Nilituma ujumbe mfupi kwa watu hawakuja akakimbia. Siku ya pili alikuja tena ila hakukaa sana," anaeleza.

Anasema kabla ya mtuhumiwa kuja kwake, alipokea taarifa za wananchi wawili, mmoja akieleza kijana huyo alikwenda kwake kumtishia na mwingine akitaarifu tukio la wizi alilofanya mtuhumiwa huyo nyumbani kwake kwa kumwibia wali aliokuwa akipika.

"Mwananchi wa kwanza alikuwa baba wa kijana ambaye alikuwa na urafiki na mtuhumiwa. Huyu baba alikuja kwangu Jumanne kunieleza mtuhumiwa huyu amekwenda kwake na kumtishia akimwambia amuonye mtoto wake asifanye mazoea naye atamfanyia kitu kibaya.

"Siku iliyofuata (Jumatano usiku) alikuja mwanamume wakati huo tukiwa ndani tukihofia mtuhumiwa, akanigongea sikufungua bali tukawa tunaongea akiwa nje. Akanijulisha mtuhumiwa amekwenda kwake na kuchukua sufuria la wali alilokuwa ameinjika jikoni na kutokomea nalo. Alikuwa ameshika panga.

"Baada ya ripoti hii alipoondoka, mtuhumiwa alifika kwangu akakaa nje ya ua wangu akiwa na sufuria akawa anakula, alikuwa ameshika panga, sikuweza kutoka. Hakusema chochote zaidi baada ya kula akawa anazunguka nyumba yangu kwa kupiga panga ukutani na juu ya bati la nyumba yangu kututishia.

"Niliandika ujumbe mfupi kwa majirani na kwa diwani, lakini kila mmoja alikuwa muoga kutoka. Mtuhumiwa alikaa kwangu takribani saa nane, akiendelea na vitisho hivyo kutoka saa mbili usiku hadi saa tisa usiku anaondoka," anasimulia.

Anasema siku iliyofuata wale aliowatumia ujumbe akiwamo diwani walifika kumpa pole na ndipo alipomwomba kijana mmoja wa jirani alale hapo nyumbani kuongeza nguvu endapo atarudi.

"Usiku wa kuamkia Ijumaa (juzi) mtuhumiwa alirudi tena nyumbani kwangu na akaendelea kutishia, lakini hakuna alichokuwa akisema. Hii siku hakukaa sana, akaondoka," anasimulia.

Muhanuka anasema huyo kijana awali alikuwa akiishi Dar es Salaam na miaka mitano iliyopita alirudi kwa baba yake kijijini hapo na amekuwa akijishughulisha na shughuli za shamba, hivyo muda mwingi hushinda shambani.

Hata hivyo, Mwenyekiti huyo anasema, licha ya taarifa kutolewa polisi, lakini hadi sasa hawaoni juhudi zozote za kumsaka mtuhumiwa huyo ambaye anatishia maisha ya wananchi.

**BABA WA MTUHUMIWA**

Baba mzazi wa mtuhumiwa, Mandanga Sultani, anasema hajamwona muda mrefu mtoto wake ambaye huishi shambani muda wote akijishughulisha na kilimo.

"Mimi ndiye mzazi wa huyu Ismail, umri wake ni miaka 26 kuendelea. Tukio ni kweli limetokea na si la kuficha. Kafanya tukio hilo mpaka sasa tupo kwenye msako na kwenye uongozi wa kijiji nimeshatoa ruhusa uamuzi wowote watakaoamua wafanye juu yake.

"Nimesema mtoto simba siwezi kumficha ndani, kama mzazi nimewaambia vyovyote wamfanye, wakiamua kumpeleka mahakamani au vinginevyo ni sawa tu.

"Sielewi kwa nini kafanya tukio hili. Wanawake mbona wako wengi. Hivi unawezaje kumbaka mtoto wa miaka 10. Huyu aliyemfanyia ukatili ni mtoto wa mjomba wake. Mpaka sasa sijapata taarifa zake na jana (juzi) tulikaa kikao cha kijiji. Nyumbani kwangu hajaja kunitishia," anasema.

**TAKWIMU**

Jumatano wiki hii, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, wakati akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/25, alisema makosa ya ukatili wa kijinsia yameongezeka.

Alisema katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, makosa yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi yalikuwa ni 24,535 ikilinganishwa na makosa 21,317 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la makosa 3,218 sawa na asilimia 13.

Aidha, alisema ongezeko hili limetokana na mmomonyoko wa maadili katika jamii, hususan makosa ya ubakaji na ulawiti ambapo kesi 5,865 zimefikishwa mahakamani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kauli ya Kikwete kuhusu uongozi yafaa kuzingatiwa

**TAASISI** ya Uongozi juzi ilifanya mahafali ya saba yaliyojumuisha wahitimu 198 wa kozi ya uongozi kutoka taasisi mbalimbali za serikali na Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete alikuwa mgeni rasmi.

Katika hotuba yake, Kikwete alitoa wosia mzito si kwa wahitimu hao tu bali kwa viongozi walioko kwenye taasisi za serikali na binafsi ambao majukumu yao ya kila siku ni kuhudumia wananchi na kuwaletea maendeleo. Kikwete aliwashauri wahitimu hao kuwa na mipango na mawazo yatakayosaidia kuacha alama katika uongozi wao pale watakapoacha au kuhamishwa.

Kiongozi huyo ambaye amejijengea sifa kubwa katika uongozi tangu enzi za ujana wake, alisema ni muhimu kwa viongozi wawe na mipango kabambe kwa taasisi wanazoongoza na kwa nafasi zao ili watakapomaliza wakumbukwe kwa mazuri waliyofanya kwa kizazi cha sasa na vijavyo. Alisisitiza kwamba jambo ambalo wanapaswa kulipa kipaumbele kwenye nafasi zao za uongozi ni namna watakavyokumbukwa baada ya maisha ya uongozi na ni alama gani wataiweka ambayo haitafutika miaka mingi.

Licha ya kufanya hivyo, alisisitiza kuwa wanapaswa kuwa chimbuko la mawazo katika kutekeleza majukumu yao na pia kuwa chanzo cha mabadiliko katika ngazi mbalimbali wanazozitumikia. Pia alisema viongozi wanapaswa kuwa tayari kutafuta suluhu za changamoto zinazoendelea kama vile umaskini, mabadiliko ya tabianchi, ujinga, njaa na maradhi.

Wahenga wanasema uzee ni dawa. Maneno ya kiongozi huyo aliyeshika nyadhifa mbalimbali ndani ya chama tawala na serikali pamoja na kuwa nyota katika medani ya kimataifa, yanasadifu na ukweli kuhusu uongozi. Kiongozi siku zote anapaswa kuwa mbunifu na mstari wa mbele katika utekelezaji wa mawazo yake pamoja na kutatua changamoto zinazoihusu taasisi na jamii inayomzunguka.

Jambo hilo katika uhalisia wa sasa limekuwa kama msamiati mgumu kwa baadhi ya viongozi wa sasa. Idadi kubwa ya watu wanaoingia katika uongozi hawafikirii changamoto au matatizo yanayowasibu wananchi au jamii bali matamanio na mipango binafsi. Matokeo yake, wanashindwa kuleta mabadiliko chanya kupitia nafasi wanazopewa katika uongozi.

Kutokana na ukweli huo, watu wengi wanaosaka nafasi za uongozi wanatumia fedha ili kuzipata na kuna msemo uliozoeleka katika jamii ya sasa kwamba bila pesa ni vigumu kupata uongozi na mkono mtupu haulambwi. Kwa mantiki hiyo, wanatumia fedha kuanzia uongozi wa serikali za mitaa hadi serikali kuu kwa matumaini kwamba watavuna faida kutokana na 'uwekezaji' kwenye kura.


Katika miaka ya 1990 na 2000 waliokuwa wabunge wawili katika mkoa wa Dar es Salaam, waliwahi kuliliwa shida na wapigakura wao kuhusu kero za maji na majibu waliyotoa ni kwamba ubunge waliupata kwa fedha zao na si hisani ya wananchi hao. Huo ndio ukweli na ndiyo maana watu kama hao wanapoingia kwenye nafasi yoyote ya uongozi, mawazo yao ni kujineemesha wao na wale wanaowazunguka.

Ni wakati mwafaka sasa kwa viongozi, katika nafasi yoyote, kubadilisha fikra zao na kurejea maneno ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, kwamba uongozi ni dhamana ya kuwatumikia watu na si kutumikiwa. Kama alivyosema Kikwete viongozi wafanye mambo yatakayosaidia kutatua kero zinazowakabili wananchi ili waache alama pindi watakapoondoka.

Waasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, walitambua kuwa wamepewa dhamana ya kuwaongoza Watanzania kwa kuwatatulia kero zinazowakabili. Kwa kutambua na kutekeleza hayo, viongozi hao japokuwa wametangulia mbele ya haki, wameacha alama isiyofutika kwa vizazi vingi ndiyo maana mpaka sasa wanaendelea kukumbukwa.

Kwa mantiki hiyo, viongozi wa sasa na wajao, wanapaswa kuzingatia kauli ya Mzee Kikwete kuhusu dhana ya uongozi ili wakumbukwe baadaye kwa kazi zao njema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Watanzania ni fursa kuchangamkia daftari la wapigakura

**KAZI** ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, inatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Julai mwaka huu, huku wapigakura 4,369,531 wakitarajiwa kuboresha taarifa zao.

Lakini pia wapigakura 594,494 wanatarajiwa kuondolewa katika daftari kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kupoteza sifa za kuwa wapigakura, ambapo zoezi hilo litakapokamilika, daftari hilo linatarajiwa kuwa na wapigakura 34,746,638.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufani) Jacobs Mwambegele, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, atazindua uboreshaji wa daftari hilo mkoani Kigoma.

Vituo vitakavyotumika kwenye uboreshaji wa daftari ni 40,126, ambavyo tume hiyo ilifanya uhakiki vituo hivyo vya kuandikishia wapigakura mwaka jana na sasa kinachofuata ni kazi ya uboreshaji huo.

Binafsi nitoe wito kwa Watanzania ambao wamefikia umri wa kupigakura au kubadilisha taarifa zao, kuchangamkia fursa hiyo ya kiuboresha taarifa zao wakati ukifika.

Julai Mosi si mbali, hivyo ni muhimu kwa kila mwenye sifa ya kupiga kura ambaye taarifa zake zitakiwa kuboreshwa au ambaye amefikisha umri wa miaka 18 ajiandae kujiandikisha ili wakati wa uchaguzi kushiriki.

Ni vyema Watanzania waitumie fursa hiyo vizuri wakiwamo ambao wamehama kutoka mkoa au wilaya moja kwenda nyingine ili wabadilishe taarifa zao wawe na haki kushiriki uchaguzi.

Vilevile, ni fursa kwa waliohama kata na majimbo kurekebisha taarifa zao zikiwamo za majina na nyingine, kwani ni haki ya kila Mtanzania wa kuanzia miaka 18 mwenye akili timamu kuchagua au kuchagua.

Pamoja na hayo, ninaona kama muda wa kuanza kuboresha daftari hilo ni mfupi hasa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Ikumbukwe kuwa, kuanzia Julai mosi mwaka huu wakati daftari hilo litakapoanza kuboreshwa hadi Oktoba, ni miezi minne. Je itatosha kuwafikia Watanzania wote na kuwaandikisha?

Sina tatizo na uchaguzi mkuu wa mwaka kesho, kwa sababu kuanzia Julai mosi mwaka huu hadi kufikia uchaguzi huo, ni mwaka mmoja na miezi kadhaa, hivyo inawezakana walengwa wote wakafikiwa.

Nakumbuka mwaka 2015 wakati wa kuandikisha wapigakura, kulikuwa na tatizo la mashine la BVR kuharibika mara kwa mara. Sijui kama tatizo hilo halitajirudia katika uboreshaji unaotarajia kuanza Julai Mosi.

Hata kama mashine hizo hazitakuwa na matatizo, lakini ninaona kama miezi iliosalia hadi kufikia uchaguzi wa serikali za mitaa ni michache ikilikangishwa na ukubwa wa nchi hii na jiografia yake.

Sawa, vituo vya kuandikisha wapigakura vimeongezeka kutoka 37,814 vilivyotumika kuandikisha wapigakura mwaka 2019/2020 hadi kufikia 40,126, vitakavyotumika kuboreshea daftari mwaka 2024/25.

Lakini inawezekana kazi ikawa kubwa na hata kusababisha baadhi ya watu waliofikisha umri kupigakura katika uchaguzi wa serikali za mitaa wasifikiwe kirahisi kutokana na muda na jiografia ya nchi kama nilivyoeleza, kwani baadhi ya maeneo ya nchi hayafikiki kirahisi.

Pamoja na hayo, niwahimize tena Watanzania, kwamba waitumie fursa hiyo vizuri wakiwamo walioandikishwa awali na sasa wamehama kutoka mkoa au wilaya moja kwenda nyingine, ili wahamishe taarifa zao.

Vilevile ni fursa kwa wale waliohama kata na majimbo kurekebisha taarifa zao, yakiwamo majina na taarifa nyingine muhimu, ingawa ninaona muda uliopo ni mfupi hasa kwa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Mwenyekiti wa tume hiyo ameshaweka wazi kuwa vituo vilivyopo vya kuboreshea daftari hilo ni 40,126, huku vya Tanzania Bara vikiwa 39,709 na Zanzibar 417.

FIKRA MBADALA

# Chanzo cha ubaguzi ni ukosefu elimu ya uraia



Pascal Mayalla

HIVI karibuni, kumeibuka hoja za kibaguzi za baadhi ya wanasiasa kwa kutoa kauli za kuwanyooshea watu vidole na kuwaita "wao Wazanzibari", "sisi Watanganyika".

Miongozi mwa watu wanaotoa kauli hizi ni viongozi wa vyama vya upinzani, waliofilisika kisiasa na baadhi ya wanaolaani kauli hizo ni baadhi ya viongozi wa chama tawala. Nimemsikia mmoja wa viongozi hao, akilaani vikali kauli hizo bungeni kwa maneno makali kabisa. Huko pia ni kufilisika kisiasa.

Aliyesema wanasiasa wanaojinasibisha na Utanganyika na Uzanzibari, dini zao, kanda zao, au makabila yao, ni watu muflisi, waliofilisika kisiasa, ni Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na akaiandikia kitabu kinaitwa "Nyufa". Mwalimu alisema dhambi ya ubaguzi ni mbaya sana, ni kama kula nyama ya mtu. Ukiishakula huwezi kuacha!

Uraia ni hoja ya kikatiba na kisheria. Kabla ya Muungano, tulikuwa na nchi mbili za Tanganyika na Zanzibar, hivyo tulikuwa na uraia wa Tanganyika na uraia wa Zanzibar. Baada ya Muungano, tukaungana kuwa nchi moja ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa na uraia mmoja tu wa Tanzania.

Baada ya Muungano, majina ya nchi hizi zote mbili, Tanganyika na Zanzibar, yalibadilika na kuwa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, hivyo jina la Tanganyika likafutwa ila jina la Zanzibar liliendelea kuwepo kutokana na uadimu na uadhimu wa huu Muungano wetu.

Uadimu wa Muungano

Miungano ya nchi zote duniani ni miungano ya aina mbili kuu. Kwanza ni Muungano wa 'Union'. Katika aina hii ya Muungano, nchi mbili zinaungana na kuunda nchi moja. Zile nchi zote mbili zilizoungana, zote zinakufa na kuunda nchi moja mpya. Hivyo ndivyo ulivyo muungano wetu kimataifa. Tanganyika na Zanzibar zimekufa na umezaliwa nchi moja mpya ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, yenye uraia mmoja wa Tanzania. Hakuna tena uraia wa Tanganyika wala wa Zanzibar bali kuna uraia mmoja wa Tanzania.

Tanganyika haipo nafasi yake imechukuliwa na Tanzania Bara na Zanzibar japo ipo, si nchi bali ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yenye utawala wake wa ndani lakini hakuna uraia wa Zanzibar. Kama nilivyosema awali, uraia ni mmoja tu wa Tanzania.

Pili, Muungano wa shirikisho. Aina hii ya Muungano, nchi mbili au zaidi zinaungano kuwa nchi moja, lakini zinaendelea kuwa utawala wa ndani na serikali zao, chini ya utawala mkuu wa nchi ya serikali ya shirikisho, kama Marekani.

Vivyo hivyo, muungano wetu kwa ndani ni wa shirikisho wenye nchi mbili, Tanzania na Zanzibar, yenye marais wawili, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), mabunge mawili, Bunge la JMT na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, zenye mahakama mbili, Mahakama ya JMT na Mahakama ya Zanzibar.

Pamoja na yote hayo, kwenye uraia, bado ni mmoja tu wa JMT lakini kwa Zanziar, wana ukaazi na si uraia bali ni utambulisho tu wa wakaazi wa Zanzibar lakini wote ni Watanzania.

Hivyo, Muungano wa Tanzania ni adimu pekee duniani ambao kwa upande mmoja ni muungano wa 'union' na upande wa pili ni muungano wa shirikisho. Hakuna muungano wa aina hii popote duniani.

Uadhimu wa Muungano

Muungano wetu licha ya kuwa ni adimu, pia ni adhimu, wenye dhima ya kuungana milele. Miungano yote duniani, inaundwa kwa mikataba ya kisheria ya muungano. Mikataba hiyo inakuwa na kipengele cha jinsi ya kuivunja miungano hiyo. Kwenye zile 'Articles of Union' za Muungano wetu, hakuna kipengele cha jinsi ya kuuvunja Muungano, hivyo zile Hati za Muungano si mkataba wa muungano bali ni makubaliano ya Muungano yenye dhima ya muungano wa milele ndiyo maana tunasema "Muungano tutaulinda kwa gharama yoyote".

Tangu tumeungana na tangu nimezaliwa na kupata akili, sikumbuki hata mara moja kusikia vipindi vya elimu ya uraia kuhuhusu huu muungano wetu adimu na adhimu, hali inayosababisha baadhi ya Watanzania kuanza kujinasibisha na utanganyika wao na uzanzibari wao.

Kwa vile Tanganyika ilifutwa na jina la Tanganyika kufutwa, utanganyika nao ukafutika. Watanganyika tunajisabisha kwa utanzania wetu, lakini kwa vile jina la Zanzibar halikufutwa na kuna uzanzibari ukaazi, hivyo baadhi ya Wanzanzibari wanajinasibisha kwa uzanzibari wao kama uraia wa Zanzibar, badala ya kujinasibisha na Utanzania wao.

Kungekuwa na vipindi vya elimu ya uraia kuhusu katiba, sheria, haki na wajibu, kusingekuweao vitimbakwiri wowote, wanaojinasibisha kwa utanganyika wao au uzanzibari wao kwa sababu uraia wa JMT ni mmoja tu. Hakuna uraia wa Tanganyika wala uraia wa Zanzibar.

Wiki ijayo, nitaendelea na kuwaletea hizi chokochoko za kuuchokoa Muungano na kuanza kunyoosheasha vidole vya ubaguzi wa "Utanganyika na Uzanzibari" zilianzia wapi, dawa yake ni nini na tiba ya kudumu ya kuitibu sumu hii na kuiangamiza kabisa.

**Paskali**
**0784270403**

**Pili, Muungano wa shirikisho. Aina hii ya Muungano, nchi mbili au zaidi zinaungano kuwa nchi moja, lakini zinaendelea kuwa utawala wa ndani na serikali zao, chini ya utawala mkuu wa nchi ya serikali ya shirikisho, kama Marekani.**

# Akutwa amejinyonga kwa kutumia mtandio

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKAZI wa Muheza, wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, Zawadi Samwel (21), amekutwa amejinyonga kwa kutumia mtandio wake.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Muhudhwari Msuya, aliwaambia waandishi wa habari ofisini kwake jana kuwa Zawadi alikutwa akininginia chumbani kwake.

Msuya alisema tukio hilo lilitokea Mei 16, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana eneo la Muheza, Maili Moja wilayani Kibaha.

Kaimu kamanda huyo alisema chanzo cha kujinyonga ni ugomvi kati yake na wifi yake baada ya kupatwa na hasira, hivyo kuchukua uamuzi huo.

Akizungumzia tukio hilo, alisema Zawadi alikutwa ananing'inia chumbani kwake na wakati anatekeleza azma yake hiyo alikuwa peke yake nyumbani.


"Jeshi bado linaendelea na uchunguzi kuhusiana na tukio hili. Mara baada ya uchunguzi wa awali, mwili ulikabidhiwa kwa ndugu ili kuendelea na taratibu za mazishi," alisema Msuya.

Mwenyekiti wa Shina Namba 3, Mtaa wa Muheza, Sudi Bakari, alisema Zawadi alikuwa akiishi katika eneo hilo na kaka yake ambaye wakati tukio likitokea yeye na mke wake hawakuwapo.

Bakari aliiambia Nipashe kwa njia ya simu kwamba Zawadi alifika katika mtaa huo kuishi nyumbani kwa kaka yake ambaye alikuwa anaishi na mke wake.

Kiongozi huyo wa shina alisema wakati tukio hilo linatokea, wifi wa marehemu hakuwa nyumbani na alipoorudi baada ya kushuhudia tukio hilo, aliwaita majirani na baadaye kumwarifu mwenyekiti wa shina ambaye alitoa taarifa kwa mamlaka husika.

Taarifa kutoka kwa mmoja wa wananchi wa mtaa huo (jina limehifadhiwa) zilisema Zawadi amefariki dunia akiwa na ujeuzito na kwamba kulikuwa na kutokuelewana kati yake na wifi yake.



# Majaliwa asisitiza umuhimu kufanya mazoezi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesisitiza Watanzania kuendelea kujiwekea utaratibu wa kufanya mazoezi kwa kuwa ndiyo njia sahihi ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza.

Amesema takwimu za Wizara ya Afya zinaonyesha hospitali zina idadi kubwa ya wagonjwa wenye magonjwa yasiyoambukiza, hivyo hamasa na msisitizo uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan wa kufanya mazoezi hauna budi kupewa kipaumbele na wananchi wote.

Majaliwa alitoa wito huo jana katika Mbio za Pugu (Pugu Marathon) zilizolenga kuendeleza kituo cha Hija cha Pugu kilichoanzishwa na Wamisionari wa Shirika la Wabenediktini kutoka Ujerumani waliofika Dar es Salaam mwaka 1888 kuwa kituo cha kimataifa.

"Pamoja na kusisitiza mazoezi kama moja ya njia ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa, tuendelee kuelimishana pia kuhusu ulaji sahihi wa vyakula na kubadili mitindo ya maisha ambayo ina athari katika afya zetu," alisema.

Waziri Mkuu amezielekeza taasisi za serikali, dini na binafsi kuweka utaratibu wa kuhamasisha wananchi katika maeneo yao kushiriki katika mazoezi ambayo yanatumika kujiimarisha wenyewe kiafya na kusaidia wahitaji mbalimbali.

Alitumia fursa hiyo kuwasisitiza wataalamu wa afya na lishe washiriki katika matukio hayo na waongeze juhudi za kuelimisha jamii kuhusu magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa michezo na mazoezi ni miongoni mwa kinga kubwa.

Awali, Askofu Msaidizi wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Stephano Musomba, alisema katika mbio hizo, zaidi ya watu 7,000 walishiriki na Sh. milioni 300 zilikusanywa. Fedha hizo zinatarajiwa kutumika katika kuendeleza kituo cha hija cha Pugu.

Askofu Musomba pia alitumia fursa hiyo kuwasisitiza Watanzania waendelee kufanya kazi kwa bidii ili kukuza uchumi wa Taifa na mtu mmoja mmoja.

"Kufanya kazi si adhabu, kazi ni kipimo cha utu," alisema.



Akitokea Pugu, Waziri Mkuu alisimama katika eneo la Gongolamboto na kusalimia wananchi na kusisitiza waendelee kuiunga mkono serikali kwa kuwa Rais Samia Samia anaguswa na maisha ya Watanzania na anataka kuona watanzania wanahudumiwa.

Aidha, Majaliwa aliwaeleza wakazi hao kuwa serikali iko imara na inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuangalia mahitaji ya kila eneo nchini na kuyafanyia kazi ikiwemo miundombinu ya barabara.

# Naibu Waziri ataka uungwaji mkono mapambano mmomonyoko wa maadili

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mwanaidi Khamis ameweka msisitizo kwa kuliomba Bunge na Jamii kwa ujumla kuunga mkono jitihada za mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na mmomonyoko wa maadili.

Mwanaidi aliyasema hayo juzi wakati akijibu hoja mbalimbali za wabunge waliochangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2024/25, bungeni jijini Dodoma.

Alisema serikali kupitia wizara hiyo inaratibu na kusimamia afua za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ambazo ni msingi muhimu katika ukuaji ili kujenga familia na taifa lenye maadili mema.

Aliiomba jamii kuzingatia suala la malezi kwa watoto kwa kuhakikisha wanapata muda wa kukaa na kuzungumza nao kuhusu masuala na changamoto mbalimbali zilizopo kwa wakati huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Katika kuhakikisha mtoto analindwa na vitendo vya ukatili na mmomonyoko wa maadili, alisema wizara kwa kushirikiana na wizara za kisekta inaendelea kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazogusa suala la mtoto.

"Wizara yetu kwa kushirikiana na wizara zingine kama Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Katiba na Sheria itajadiliana na kuona namna ya kuwa na Sheria itayomlinda mtoto moja kwa moja na matumizi ya mitandao" aliesisitiza.

Kuhusu ustawi wa wazee nchini, Naibu Waziri Mwanaidi amesema wizara iko katika hatua ya mwisho ya kurekebisha Sera ya Wazee ili kuendana na wakati uliopo na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili wazee nchini.

"Mambo muhimu yanayozingatiwa katika sera hiyo ni kutoa elimu ya wazee kujiandaa kustaafu, huduma za afya, msaada ya kisaikolojia, mazingira wezeshi, uwezeshaji wa wazee katika mabadiliko ya teknolojia yaliyopo," alisema.

Kuhusu mashirika yasiyo ya kiserikali, alisema wizara inaendelea kuyaratibu na imeanzisha ramani ya kidijitali itakayosaidia kutambua mashirika hayo yalipo na yanafanya shughuli gani, ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, wakati wa Jukwaa la Mwaka la NGO 2023.

Bunge lilipitisha makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha Sh. bilioni 67.9.




Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (wa pili kulia), akikabidhi mtungi wa Taifa Gesi kwa Kiongozi wa kimila wa kabila la Kimasai, Laigwanani Komba Riko wakati wa hafla ya kukabidhi mitungi 150 ya gesi bure kwa wananchi wa Kijiji cha Msomela, wilayani Handeni, mkoani Tanga jana, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono Kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama mzigo wa kuni na kutumia nishati safi ya gesi pamoja na kuhifadhi mazingira. Wengine ni Meneja Mkuu wa Taifa Gesi, Davis Deogratius (kulia), Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Wakili Albart Msando (wa tatu kulia) na Mwenyekiti wa kijiji hicho, Thomas Sindilo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Serikaki yaweka mikakati kuzuia uhaba mafuta

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeweka mikakati kuhakikisha mafuta ya kula yanayoweza kupatikana nchini yasiagizwe nje kwa kutekeleza ujenzi wa viwanda vya kuchakata malighafi hiyo.

Viwanda hivyo ni vya Kigoma kinachotoa mafuta ya Mawese na Pwani ambacho kitakuwa na uwezo wa kukamua kila aina ya zao linalotoa mafuta.

Hayo yalisemwa juzi Dar es Salaam wakati wa hafla ya utiaji saini ya ushirikiano baina ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Exim, ambayo imepewa dhamana ya asilimia 70 iliyowawezesha kutenga Sh. bilioni 30 kwa ajili ya kuwakopesha wakulima kwa kipindi cha miaka mitano.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na washirika wao, kumekuwako na changamoto kwenye viwanda kwa kuwa vilivyoko vina uwezo wa kukamua zao moja la mafuta jambo linalochangia uhaba kipindi ambacho si msimu wa zao husika.

"Utafiti uligundua kwamba kiwanda ambacho kinachakata alizeti, msimu unapofika kama una miezi minne, uwezekano wa kukosa malighafi kwa miezi minane iliyobaki ni mkubwa, hivyo wazo lililoko ni kutengeza viwanda vyenye uwezo wa kuchakata mazao yote kwa misimu yote na cha Pwani kiko katika hatua za mwisho.

"Tutahakikisha mafuta ya kula yanapatikana kwa wingi. Katika taifa letu tumebarikiwa kuwa na ardhi kubwa na yenye rutuba tutalima. Wakulima wadogo awali walikuwa wanapata changamoto ya soko kwa hiyo tunapotengeneza viwanda vitaenda kusaidia suala la uhakika wa soko," alisema Nyabundege.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wakulima wananufaika na kilimo wanahakikisha mikopo wanayopatiwa inakuwa katika mnyororo wa thamani kuanzia hatua ya kwanza ya uzalishaji hadi mauzo, kwa kuwaunganisha na wanunuzi.

Pia alisema serikali imekuwa ikiwapatia miongozo kuhakikisha kwamba vijana wanaojihusisha na kilimo wasifanye kwa kubahatisha, na kwamba kwa sasa uhaba wa soko la kuuzia bidha za kilimo haliko tena, huku changamoto mbalimbali zinazokabili sekta hiyo zikiendelea kutatuliwa.

Alisema ni tamanio la Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona watu wote wanaojihusisha na kilimo wananufaika, kwa kuongeza bajeti ya sekta hiyo kutoka Sh. bilioni 940 mpaka trilioni 1.2 pamoja na Wizara ya Mifugo Uvuvi ambayo imeongezeka kwa asilima 63 na kufikia Sh. milioni 460.

"Maana ya serikali kuongeza bajeti hizi inakwenda kuongeza miundombinu ili wakulima waendelee kupata nafasi ya kulima, Wizara ya Kilimo inatengeneza miundombinu ya umwagiliaji na itawawezesha kulima kutoka msimu mmoja hadi mitatu, ndiyo maana hata benki imeongezewa mitaji kwasababu wakulima wanahitaji fedha za kutosha kulima," alisema Nyabundege.

Mkurugenzi wa Fedha wa Exim, Shani Kinswaga, alisema ushirikiano huo utasaidia wakulima kutoka kwenye kilimo cha kijikimu na kufanya cha kibiashara, pamoja na kuongeza tija kubwa kiuchumi na kimaendeleo kwa ambao wamekuwa wakikosa fursa za kifedha kutokana na masharti ya kuleta dhamana licha ya kuwa na vigezo vingine.

"Tunaamini ushirikiano huu utaongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wanaoshirikiana na wizara ya kilimo hasa wale walioko ngazi za chini vijijini, tunaamini katika ushirikishwaji wa kifedha kwa makundi yote bila ubaguzi," alisema.

# MAISHA

MEI 19, 2024
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

**'CHICKEN WINGS' vipapatio vya kuku**



Ukurasa 14

## NYUMBA:
Mbinu za kupambana na mchwa kwenye nyumba



## HARUSI


Ukurasa 12




# NG'ARISHA MENO

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | ■ | C | H | A | M | A |
| H | ■ | ■ | ■ | D | ■ | S |
| A | ■ | T | U | A | ■ | T |
| G | U | U | ■ | B | A | A |
| U | ■ | M | B | U | ■ | A |
| Z | ■ | B | ■ | ■ | ■ | F |
| I | B | A | K | I | ■ | U |

## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI, WEKA KIVULI KWENYE KILA NUKTA ILI UJUE NI NANI AMEFICHWA KATIKA MAUMBO HAYA.




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


BUU, NAE, WAO SAA, SWALA, UJAZO, AGUSE, BONDA, THAWABU, ASTAAFU

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya Adaktari

MTOTO Grace alikuwa akitembea juu ya sakafu ya marumaru kwa mwendo wa haraka, mama yake alimwangalia na huku akiwa na hofu asije akateleza na kuanguka chini.

Mama: Grace unakimbilia wapi, hujui kama unatembea kwenye marumaru?

Grace: Mama nakwenda kuchukua kitabu changu cha hadithi Juma ameniibia.

Mama: Lakini kuwa mwangalifu, usije ukaumia na mimi sina pesa ya kukupeleka hospitali.

Grace: Lakini mama kule shuleni mwalimu alitufundisha kwamba 'kuteleza si kuanguka', hivyo sina hofu.

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu alitaka kuwajenga muwe na ujasiri wa kufanya jambo ambalo awali umeshindwa.

SWALI

Taja aina tatu ya wanyama wa jamii ya swala wanaopatikana porini.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi- 3

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vipengele vingine vyanzo vya matatizo ya ndoa nyingi. Hii ni sehemu ya tatu na ya mwisho katika eneo hilo.

Tayari nimejadili vyanzo kadhaa labda kwa faida ya wale ambao hawakubahatika kusoma safu hii nao wapate mwanga kidogo. Nilitaja ndoa zilizofanyika pasipo Mungu kuhusika(wakati ulikuwa adui wa Mungu).

Kingine ndoa kwa sababu ya kupata mimba kwa bahati mbaya, kujihusisha kimapenzi kabla ya ndoa, ndoa zilizofungwa baada ya mtu kwenda kwa mganga wa kienyeji, ndoa zilizofungwa kwa shinikizo la wazazi.

Chanzo kingine kulawitiwa/kubakwa wakati wa udogo, ndoa ambazo wahusika waliwahi kufanya agano la damu na mtu mwingine (Agano la Amini). Pia ndoa zilizojengwa katika misingi ya bora kuolewa/kuoa kuliko kuishi hivi hivi.

Msomaji wangu, leo tumalizie vyanzo vingine nilivyoweza kukuandalia kwenye safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Kipo chanzo ndoa zilizojengwa katika misingi ya muonekano wa nje. Muonekano wa nje hauwezi kukufanya uwe na ndoa ya kudumu.

Mara zote uzuri wa mtu hupotea kadiri siku zinavyoaidi kwenda mbele. Wanawake wengi wana tabia ya kusema, 'bado natafuta mwanaume, awe mzuri, mrefu. Na kama mwanaume hana mwonekano mzuri siwezi kukubali anioe".

Sawa, unaweza kutafuta warembo wa kila namna, lakini ujue kwamba uzuri/mwonekano wa nje hupotea baada ya muda fulani. Utakapopotea, ndipo chanzo cha matatizo ya ndoa huanza.

Chanzo kingine ni ndoa zilizojengwa katika misingi ya mali. Kama ndoa yako imejengwa katika misingi ya mali, haitaweza kudumu. Ni vizuri kuishi maisha mazuri, lakini utajiri na mali ni vitu vya kupita. Hutaweza kujenga msingi wa ndoa yako katika mali!

Kama kuna wanawake wa kuwahurumia, ni wale wanaozunguka na kutangaza, "mtu atakayenioa anatakiwa awe mtu tajiri, awe na angalau magari mawili, awe na akaunti kama sita hizi za benki.

Siwezi kuolewa na mtu anayeishi nyumba ya kupanga. Lazima awe na uwezo wa kusafiri nchi za nje kwa ajili ya kufurahia. Sitaki mateso! Tamaa za namna hii zitakufanya ujikute unaingia katika makosa makubwa sana.

Pia wapo vijana wa kiume ambao hutafuta wanawake wenye uwezo wa magari, kazi nzuri. Wanapoona wanawake wa aina hii huanza maombi. Baada ya siku chache huja na maono kuwa wameoneshwa.

Kwa kutokujali hujikuta wameoa wanawake ambao watawafanya wasiwe na hatma nzuri ya maisha yao. Mara nyingi wanawake wa aina hiyo wanakuwa ni wale waliokata tamaa ya kusubiri kuolewa.

Hivyo, kijana yoyote atakayekuja mbele yao ni hiari yao. Hawa hujikuta wameingia katika kifungo pasipo wao kufahamu.

Ndoa zilizojengwa katika misingi ya unabii wa kishetani. Ninapoongelea unabii wa kishetani haimaanishi kutembelea waganga wa kienyeji, au wapiga ramli.

Hapa ninamaanisha kuna watu ambao wanahudhuria kwenye majengo ya manabii wa uwongo ambao hujifanya malaika wa nuru ili waue hatma za vijana.

Wao hupenda kusema, "bwana amesema, utakapokuwa unakwenda utakutana na mke wako chini ya mti kesho, umfuate huyo ndiye mke wako ambaye bwana amekuchagulia".

Hapo mtu atachanganyikiwa; maana hatafahamu ni mti upi anatakiwa kukutana na huyo mke/mume atakayefunga naye ndoa; na hivi ndivyo watu wengi wamejikuta wakioa mabomu.

Ni kweli watumishi wa Mungu wana sehemu ya kukushauri juu ya mwanamke/mwanaume unayetaka kufunga naye ndoa. Lakini unatakiwa kuwa makini maana nyakati za leo wapo watu wanaojiita watumishi wa Mungu kumbe siyo. Unaweza kujikuta umeunganishwa na mtu asiye sahihi na hatma yako yote ikapindishwa!

Ndoa zilizojengwa katika misingi ya kumilikishwa mke/mume katika umri mdogo. Ni kitendo kinachofanyika sana katika baadhi ya nchi za Afrika.

Wazazi humposa/humtoa binti yao akiwa na umri mdogo sana miaka 13 au 15 kuolewa na mtu tajiri katika jamii hiyo, au humpa mtemi. Binti huyo hutunzwa na kulelewa katika nyumba ya mumewe mpaka atakapokua.

Msingi wa mwisho kwa leo ni ndoa za mitala/wake wengi. Wanawake wengi hujikuta wameingia katika ndoa za wake wengi kwa kusukumwa. Baada ya muda wanatafuta njia kujinasua katika ndoa hiyo.

***Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581. Namba ipo pia WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Wameng'ooka KIA sawa, uwanja unalindwaje?

NAKUBALIANA na hoja ya Msemaji Mkuu wa Serikali, Mohbare Matinyi, kuhusiana na uamuzi wa kuwaondoa wananchi katika ardhi inayomilikiwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Pamoja na kukubaliana huko, nina maswali hayaishi kichwani.

Hakuna ubishi kwamba kaya zilizoko ndani ya eneo hilo la ardhi ya KIA ni 1,712 za vijiji vinane vya mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Kama hoja ni kuwaondoa kwa sababu ya vumbi kubwa la upepo wa kisulisuli linalotimka, kuathiri miruko na utuaji wa ndege kiasi cha ndege kushindwa kutua na kwenda nchi jirani, je, tatizo litakuwa limekwisha?

Nani alifumba macho, akawaacha wakaingia katika ardhi hiyo na kuwaacha wakajenga makazi, wakaanzisha shughuli za kiuchumi kama ufugaji na kilimo ili alaumiwe?

Hilo eneo kwa sasa litalindwaje ili kutoruhusu wananchi, hasa wa jamii ya kigugaji ya Kimasai kutoingiza mifugo yao na kuendelea kuathiri utoto wa asili na mazingira yake.

Miongoni mwa athari pia ni shughuli za kibinadamu kusababisha kuharibika kwa uoto wa asili kwa kukata miti, majani na kulisha mifugo na pia kusababisha serikali kushindwa kutekeleza mpango wake mahususi kwa ajili ya kuendeleza uwanja huu.

Taarifa ya serikali inaeleza kwamba uwanja wa KIA ulivamiwa na wananchi wa wilaya za Hai (Kilimanjaro) na Arumeru (Arusha) kati ya mwaka 2007 hadi 2010.

Lakini taarifa hiyo hiyo, inasema uwanja huo ulianza kumilikiwa na serikali mwaka 1969 wakati huo ukiwa chini ya Pori Tengefu la Sanya Lelatema, lililokuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 800.

Katika eneo hilo, inaelezwa kuwa serikali ilitenga kilomita za mraba 110 kutoka kwenye hizo 800 mahusus kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huo na baadaye na eneo lilipimwa rasmi mwaka 1989 kwa ramani iliyokuwa na namba E 5255/18 kisha ukasajiliwa na kupewa namba 231264 na hatimaye hati ilipotoka ilianza kumilikiwa ikiwa na hati 22270.

Wavamizi wanatoka vijiji vinne vya wilaya ya Arumeru ambavyo ni Kaloleni, Samaria, Malula na Majengo Kati na upande wa wilaya ya Hai, kuna vijiji vinne ambavyo ni Sanya Station, Tindigani, Chemka na Mtakuja.

Katika taarifa hiyo ya serikali, wilaya ya Arumeru wananchi wamelipwa fidia zaidi ya Sh. bilioni 4.042, wakati wilaya ya Hai wamelipwa Sh. bilioni 7.27 zilizojumuisha fidia ya majengo, mazao ya kudumu, posho ya makazi, posho ya usafiri, posho ya usumbufu na posho za makaburi.

Mpaka kufikia Mei 14, mwaka huu, wananchi 46 pekee ndio ambao bado hawajalipwa malipo yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa akaunti za benki, majina kutofautina yaliyoko katika taarifa za malipo na yaliyoko benki.

Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, kuna tatizo la kukosekana kwa uthibitisho wa mirathi kwa wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia na baadhi ya wananchi kufungua mashauri ya madai Mahakama Kuu, kupinga ulipaji unaoendelea.

Haiingii akilini unawaacha watu wanavamia uwanja, wanajenga makazi ya kudumu, halafu ndipo serikali inaamka. Hivi hamkuwaona wakati wanajenga ndani ya uwanja?

Nakumbuka Agosti, 2014 kamati ya usuluhishi iliyoundwa na aliyekuwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda (wakati huo), kwa ajili ya kutafuta mwafaka wa mgogoro wa ardhi kati ya wakazi wa vijiji hivyo vinane, ilishindwa kutekeleza jukumu hilo baada ya wanavijiji hao kukataa wazo la kutaka kuwekwa upya kwa alama za mipaka ya ardhi.

Wakati huo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alikuwa Prof. Anna Tibaijuka, ambaye alipambana kufa na kupona kuwahamisha katika makazi yao wananchi hao bila mafanikio.

Hoja ya Tibaijuka ilikuwa kupisha upanuzi wa uwanja huo kabla ya serikali kutumia nguvu. Leo Rais Samia Suluhu Hassan kafanikiwa kutumia diplomasia, kuwalipa fidia na wameondoka kwa hiari. Tunamshukuru kwa wema huo.

Sasa, kama ndivyo, ili kubakiza hai malengo ya uendekezaji wa uwanja wa KIA, ni lazima maeneo yake yadhibitiwe kwa namna yeyote ile, yasiendelee kuvamiwa.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***







Ni kumbukum-bu isiyosahau-lika kwa Thabith Chumwi Zakaria katika maisha yake wakati alipoanzisha familia miaka mi-nane iliyopita. Mungu ai-





# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## TUPIA MIWANI

MIWANI ni miongoni mwa pambo linalopendwa na watu kwa ajili ya kunogesha na kuongeza mvuto.

Wanawake na wanaume wamekuwa wakivaa miwani baada ya kutupia mavazi makali wakiwa katika shughuli zao za kila siku.

Miwani yapo ya aina mbalimbali, lakini leo tutazungumzia jinsi ya kutumia mawani ya kawaida inayovaliwa na watu wa rika tofauti hasa vijana.

Miwani ya aina hii imepata umaarufu baada ya vijana kuyatumia kama aina ya mapambo ili kuwaongezea mvuto.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanasema mwanaume anapovaa miwani ya aina hii anaonekana kuwa mtanashati, mtulivu na mwenye kujitambua.

JINSI YA KUCHAGUA

Kabla ya kuamua kutumia miwani, hakikisha unafanya chaguo sahihi kulingana na vazi unalotaka kuvaa.

Hakikisha ukubwa wa miwani yawe sawa na aina ya kichwa chako, usichukue makubwa au madogo sana kwa sababu hayatakukaa vyema na kukupa muonekano tofauti.


Baadhi ya wanaume wanavaa miwani bila kuangalia aina gani ya mitindo inayofaa, jambo hili linaelezwa ni baya kwa sababu mitindo mingine haifai kuvaliwa mbele ya jamii.

Kwa wale wanaopenda kuwa na flemu zenye rangi tofauti, unatakiwa kuhakikisha rangi za flemu zilingane na nguo unazotaka kuvaa kwa wakati huo.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# NG'ARISHA MENO



MENO ni kiungo cha kipekee katika taswira ya binadamu, yanapokuwa na afya nzuri hujenga kujiamini na uso wenye tabasamu zuri.

Iwe mwanaume au mwanamke kitu cha kwanza kama kitambulisho ni muonekano wako wa meno na kisha hufuata vitu vingine.

Ukiwa na meno yenye mwonekano mzuri na angavu, ni rahisi mtu kutabasamu, kucheka na kuongea mbele za watu.

Hata hivyo, kwa miaka mingi ni jambo la kawaida kuona watu wakipoteza mwonekano mzuri wa meno kwa kuondoa asili ya weupe na kuwa rangi ya kahawia.

Lakini kuna njia za kuzuia uharibifu wa meno kwa wanaopenda kuonyesha tabasamu kila siku.

**Tumia Limao kusafisha**

Ikiwa meno yako yanaonekana ya njano kidogo, inaweza kusababisha kubadilika rangi na kuwa meusi. Hakikisha unachukua hatua za haraka kuyatibu kabla ya kubadilika rangi.

Hatua ya kwanza chukua limao kamua maji yake weka kwenye chombo kisafi.

Chukua maji ya limao na weka mdomoni na uache kwa muda kidogo.

Baada ya dakika tano chukua mswaki na anza kusafisha taratibu meno yako.

Rudia mara tatu kwa wiki na utaanza kuona mabadiliko kwenye meno yako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# 'CHICKEN WINGS' vipapatio vya kuku



Vipapatio vya kuku ni chakula kinachopendwa na watu wengi, hasa vinapopikwa kwa ustadi wa hali ya juu.

Aina hii ya chakula kinaandaliwa kwa kuchovya kwenye mayai kisha kukaangwa kwa muda mfupi kwa kutumia siagi.

Baada ya kukaanga vinachovywa kwenye sauce na kisha kuokwa.

Zikiiva utapata ladha tamu ya vipapatio au wenyewe wanaita 'chicken wings'

Mahitaji

Vipapatio vya kuku kilo moja, yai moja pasua na vuruga, kikombe kimoja cha unga wa ngano, kwa kuweka utando (layer) juu ya kuku, kikombe kimoja cha siagi (butter).

Mahitaji mengine ni vijiko vitatu vikubwa vya soy sauce, vijiko vitatu, vikubwa vya maji safi na salama, kikombe kimoja cha sukari, nusu kikombe cha white vinegar, kijiko kidogo cha kitunguu saumu cha unga na kijiko kimoja kidogo cha chumvi.

Washa oven kwenye nyuzi joto 350 acha ipate moto.

Kata vipapatio vya kuku katikati, chovya kwenye mayai na kisha chovya kwenye unga. Hakikisha mayai na unga vimeenea vizuri.

Bandika chombo jikoni kwenye moto wa wastani, acha kipate moto kisha weka siagi. Ikiyeyuka weka vipapatio ya kuku na kaanga hadi vibadilike rangi.

Kwenye bakuli ya wastani, changanya soy sauce, maji, sukari, vinegar, kitunguu saumu, na chumvi. Koroga vizuri hadi mchanganyiko uwe sawa.

Nyunyizia sauce juu ya vipapatio vya kuku.

Weka vipapatio kwenye oven, oka kwa muda wa dakika 30 hadi 45. Weka sauce juu ya vipapatio mara kwa mara. Vikiiva epua na itakuwa tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# MBINU ZA KUPAMBANA NA MCHWA KWENYE NYUMBA

LEO tunajifunza namna ya kupambana na mchwa baada ya ujenzi wa nyumba.

Mdudu huyu amekuwa tishio kubwa katika ustawi wa nyumba na husababish uharibifu mkubwa asipodhibitiwa.

Ziko mbinu mbalimbali za kupambana na mchwa huyo baada ya kujenga nyumba ambazo zinatajwa na mtaalam Leonard Chacha.

Chacha anasema namna ya kudhibiti mchwa kwenye nyumba baada ya ujenzi kabla ya kuanza kuitumia ni lazima yote inyunyiziwe dawa ili kuua mazalia yote ya mdudu huyo.

Anasema kudhibiti mdudu huyo wakati tayari unaitumia nyumba kunaweza kusababisha usumbufu kidogo tofauti na ilivyo kwa nyumba ambayo haijaanza kutumika.

Anashauri kwamba ni vema mtumiaji au mmiliki wa nyumba kuweka utaratibu na mazoea ya kuweka dawa kila baada ya muda fulani kupita.

"Kabla ya kutumia dawa hizi za kuilinda nyumba yako dhidi ya mchwa ni vema ukapata ushauri wa mtaalamu wa ujenzi au kilimo na mifugo, kuna aina nyingi za dawa zinazotumika kwa sasa na bado nyingine zinaendelea kubuniwa kuendana na ukuaji wa sayansi na teknolojia ya utengenezaji wa dawa."

"Ni vyema kutumia dawa kwa kuzingatia maelekezo ya mtaalamu au mzalishaji wa dawa hizo kwa sababu hazifanani katika mbinu za matumizi, hivyo usiige tu kutoka kwa wengine, ni vema kupata kwanza ushauri."

Anaelekeza kwamba kabla ya kuweka dawa kwenye nyumba, unapaswa kusafisha mifereji na kuhakikisha kwamba hakuna bomba zinazovuja ikiwamo kukausha maeneo yote yenye unyevunyevu.

Pia anasema kuweka dawa kwenye maeneo yote ambayo ni njia au makazi ya mchwa, na ambayo ni chanzo hata kama hakuna mchwa wanaoonekana.

Lingine anasema ni kung'oa na kuondoa mbao zote zilizoharibiwa na mchwa na kuweka nyingine pamoja na kutoruhusu mbao zozote zigusane na udongo wowote au unyevunyevu kwa muda mrefu na kuziba matundu yote kwenye sakafu na kuta.



## Pamba meza kwa saladi



MWISHO wa juma hasa Jumapili ya leo ambayo imejaa 'vibe' la kuhitimisha msimu wa ligi ya Uingereza kwenye mchuano mkali kati ya klabu za Arsenal na Manchester City, ni vizuri ukawa na vitu vya kupendezesha nyumba yako kwa aina mbalimbali.

Nimeandika hivyo nikijua kwamba leo ni ile siku ya 'mtoto hatumwi dukani', kwa hiyo kwa wale wanaoangalia mpira kama familia unaweza kupamba meza yako kwa saladi ya matunda itawafaa sana.

Nikupe mbinu kadhaa za kutengeneza salad ya matunda kwa ajili ya kuiweka meza katika taswira nzuri na kufurahia na familia yako.

Ni kawaida kwenye familia nyingi kula aina moja ya tunda tena kipande pekee, lakini siyo vibaya siku moja moja tukaandaa mchanganyiko wenye aina tofauti za matunda.

Hivi sasa kuna upatikanaji wa parachichi kwa wingi, machungwa, mananasi, ndizi mbivu na matango; japokuwa unaweza kuandaa kwa kutumia matunda zaidi ya hayo niliyotaja yakiwamo zabibu, kiwi, papai, chenza, embe na tikiti maji. Unaweza pia kutengeneza mishikaki ya matunda mchanganyiko.

Chukua matunda yako na utakate saizi unayoitaka, kila tunda liweke kwenye sehemu yake peke yake katika sinia. Salad nzuri inapendeza ukiweka vitunguu maji.

ZINGATIA: Unaweza kuweka mayai ya kuchemsha, nyanya na mahindi mabichi yaliyochemshwa kulingana na namna ulivyokata matunda.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
'HIVI UNAJUA UNAYOYAFANYA UNAJIKUSANYIA POINTI YA MIDHAMBI?'
ULITUMWA KUNIFANYA 'KUWADI' WAKO?
KWA HAWALA
'TATIZO LA KUKURUPUKIA OFISI KUKALIA KITI ALICHOTENGULIWA MWENZAKO BILA KUPITIA KWA BABU AKUTAMBIKIE!
ZE BOSI
NINAPOKUWA NAKUAGIZA KUKU NA MCHELE WA MBEYA HUWA AKILI YAKO HAING'AMUI CHOCHOTE?
'SING'AMUI CHOCHOTE KWA KUWA DISHI LANGU MGOGORO'
POMBE ZA MKOPO HAZINA STIMU KABISA HAZIKAWII KUTOKA!
MWENZAKO HUWA NAANZAGA NA MAOMBI
BORA NIIBIWE NA 'BAAMEDI' NAJUA IPO SIKU ATANIHURUMIA LAKINI SIO VIBAKA WA RODI
BAR

## HABARI KIMATAIFA

# Gaza hali bado ngumu

**GAZA,** PALESTINA

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema halijapokea bidhaa muhimu ikiwamo vifaa vya matibabu Ukanda wa Gaza kwa siku 10, baada ya Israel kuendeleza mashambulizi katika mji wa Rafah.

Shirika hilo lilisema kuwa operesheni ya kijeshi katika mji huo unayaweka hatarini maisha ya watu wengi hasa wagonjwa.

Msemaji wa WHO, Tarik Jasarevic, alisema hatua ya Israel kufunga mpaka wa Rafah ambao unaingiza msaada ndani ya Gaza kumesababisha kuwepo kwa hali ngumu.

Jasarevic alieleza kuwa, vifaa vya mwisho vya matibabu walivyovipokea ilikuwa kabla ya Mei 6.

Aliongeza kuwa kuna hofu kutokana na ukosefu wa mafuta yanayohitajika kuzalisha nishati ili kuhakikisha vituo vya afya vinavyotoa huduma za matibabu na hospitali zifanye kazi.

"Usipokuwa na mafuta, jenereta haziwezi kufanya kazi, na usipokuwa na umeme, watu ambao wanahitaji uangalizi maalum hospitali watakuwa katika hatari. Huwezi pia kuwafanyia wanawake wajawazito upasuaji, huwezi kufanya upasuaji wowote na huwezi pia kuwahudumia watoto wachanga." alisema

Hospitali za Gaza zinahitaji hadi lita milioni 1.8 ya mafuta kila mwezi ili kuziwezesha kuendelea kufanya kazi.

Msemaji huyo alieleza kiasi lita 159,000 za mafuta pekee ndio zimeingia Rafah tangu kufungwa kwa mpaka huo ambao unatenganisha Gaza na Misri. Hospitali 13 kati ya 26 katika eneo zima la Palestina ndizo zinazofanya kazi.

Wanajeshi wa Israel walichukua udhibiti wa HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/mapambano-kati-ya-israel-na-wanamgambo-wa-hamas-yapamba-moto/a-68807044" mji wa Rafah mnamo Mei 7, kama sehemu ya operesheni yao dhidi ya kundi la wanamgambo la Hamas.

Jeshi hilo lilifunga mpaka wa Rafah ambao unatajwa kuwa muhimu kwa usafirishaji wa bidhaa na misaada ya kibinadamu kuingia ndani ya Gaza.

Wakati hayo yakijiri, jeshi la Israel lilisema kuwa raia kadhaa wa nchi hiyo walemliteketeza kwa moto lori moja lililobeba msaada katika eneo la ukingo wa Magharibi.

Vyombo vya habari vya ndani vimeripoti kuwa walowezi wa Kiisrael walihusika na shambulio hilo dhidi ya lori hilo, na kwamba dereva pamoja na wanajeshi kadhaa wa Israel walijeruhiwa katika tukio hilo.

Shambulio hilo dhidi la lori la msaada limetokea karibu na eneo la Kokhav Hashahar, yaliko makazi ya walowezi wa kiyahudi katikati mwa ukingo wa Magharibi unaokaliwa kimabavu na Israel tangu mwaka 1967.

Jumatatu, mamia ya watu walizuia na kuharibu msafara mwingine wa malori yaliyokuwa yamebeba msaada kuelekea Gaza.

Licha ya tahadhari iliyotolewa na Umoja wa Mataifa kuhusu kitisho cha njaa, mamlaka ya Israel imezuia kuingizwa kwa misaada ya kibinadamu ndani ya Gaza katika kipindi cha zaidi ya miezi saba ya vita kati yake na Hamas.

Kiwango kidogo cha msaada ndio kimeingia kupitia mpaka wa Kerem Shalom kusini mwa Gaza, wakati mpaka wa Rafah ukifungwa.

Wakati huo huo, Mshauri wa Usalama wa Taifa wa Marekani, Jake Sullivan amewasili nchini Saudi Arabia jana kujadili hali ilivyo ndani ya Gaza.

Kulingana na msemaji wa baraza hilo, Jon Kirby, alisema Sullivan atakutana na mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed Bin Salman kujadili juhudi za kupatikana kwa amani na usalama katika kanda nzima ya Mashariki ya kati.

Baada ya mkutano huo, ataelekea Israel kwa ajili ya kukutana na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu.

Kirby alisema mazungumzo yao yatajikita katika masuala ya vita katika ukanda wa Gaza, hali ya kibinadamu na makubaliano ya kuwaachia mateka wanaoshikiliwa na kundi la wanamgambo wa Hamas.

**DW**



Mashambulio ya anga ya Israel huko Jabalya, kaskazini mwa Ukanda wa Gaza yakiendelea kuteketeza majengo katika mji huo. **PICHA: AP**

# Senegal kutatua mgogoro Ecowas

**ACCRA,** GHANA

RAIS wa Ghana Nana Akufo-Addo, amemtaka kiongozi mpya wa Senegal Bassirou Diomaye Faye, kutumia nafasi yake ndani ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi ECOWAS, kusaidia kutatua migawanyiko.

Addo alisema mgogoro mkubwa unaotishia jumuiya hiyo na unaotarajiwa kushughulikiwa ni kuhusu kujitenga kwa mataifa ya Niger, Burkina Faso na Mali.

Januari mwaka huu, mataifa hayo matatu yalitangaza kujiondoa kwenye Jumuiya hiyo baada ya uanachama wao kusitishwa kufuatia mapinduzi ya kijeshi yalitokea katika mataifa hayo

Rais Faye aliesema ECOWAS, ambayo Rais wa Nigeria Ahmed Tinubu ni mwenyekiti wake, inapitia wakati mgumu lakini bado kuna matumaini ya kuwa sawa.

Nigeria na Senegal zimeahidi kuimaruisha demokrasia katika eneo hilo la Afrika Magharibi.

**DW**

**Addo alisema mgogoro mkubwa unaotishia jumuiya hiyo na unaotarajiwa kushughulikiwa ni kuhusu kujitenga kwa mataifa ya Niger, Burkina Faso na Mali.**

# RSF kuwalinda raia wanaotoka El Fasher

**DARFUR,** SUDAN

WAPIGANAJI wa kikundi cha RSF nchini Sudan, wamesema wako tayari kufungua njia salama kwa ajili ya raia kutoka katika mji wa El-Fasher ambao umekumbwa na mapigano makali.

Mji huo ambao makao makuu ya jimbo la Dafur unawaniwa na wapiganaji wa RFS, wamekuwa wakipambana na jeshi la serikali ya Sudan kwa zaidi ya mwaka moja sasa.

Kupitia ujumbe uliochapishwa kwenye mtandao wa X, wapiganaji hao walieleza kuwa wako tayari kuwasaidia raia kuondoka katika mji huo na kutafuta hifadhi katika maeneo mengine salama wanakotaka kwenda.

RSF vilevile ilisema itawapa raia wanaotaka kufanya hivyo ulinzi watakapokuwa tayari kuondoka.

El-Fasher, mji ambao raia walikuwa wamepewa hifadhi kutokana na mapigano yanayoendelea, umekuwa ikikabiliwa na mashambulizi makali kutoka kwa RSF wakiwa na nia ya kuchukua udhibiti.

Sudan imekuwa ikikabiliwa na mapigano kati ya wanajeshi wa serikali chini ya uongozi wa Abdel Fattah al-Burhan na wapiganaji wa RSF wanaoongozwa na naibu wake wa zamani Mohamed Hamdan Daglo.

Watu 15,000 wamefariki katika mapigano hayo kati mji mwingine ea Darfur wa El-Geneina peke kwa mujibu wataalam wa Umoja wa Mataifa.

Jumatano ya wiki hii, shirika la madaktari wasiokuwa na mipaka walisema kwamba hospitali yao katika mji wa kaskazini mwa Darfur ilikuwa imepokea miili ya watu zaidi ya 450 waliouawa katika mapigano yaliyoanza Mei 10.

**RFI.**

**RSF vilevile ilisema itawapa raia wanaotaka kufanya hivyo ulinzi watakapokuwa tayari kuondoka.**

MAKALA

# URAIBU KATIKA MITANDAO YA KIJAMII



Na Magabilo Masambu

**Mtoto kama anatakiwa kunyamaza anyamaze bila kutumia kitu kingine, tunadhani kwamba kwa kuwapatia simu tunaonyesha upendo wa hali ya juu mnatengeneza matatizo makubwa bila kujua.**

MACHAPISHO mbalimbali yanaeleza kuhusu Uraibu kuwa ni neno la Kiarabu ambalo kwa lugha ya kiingereza linajulikana kama "addiction" likiwa na maana ya hali inayopatikana wakati roho au mwili unahitaji mno kuwa na hisia fulani kiasi cha kuwa na matatizo katika kutekeleza shughuli mpaka kufikia tena hisia inayolengwa.

Vilevile, inaelezwa kwamba uraibu hutazamwa kama ugonjwa au utumwa wa ndani. Kwa maana rahisi ndiyo kusema uraibu ni ulevi uliopitiliza wa jambo Fulani. Mtu anakuwa hana tena uwezo wa kujizuia katika kutekeleza au kutenda jambo fulani. Hali hii ndiyo inaonekana kuikumba jami yetu katika matumizi ya mitandao ya kijamii.

Ni kweli kwamba uwApo wa mitandao ya kijamii umerahisisha shughuli nyingi katika jamii yetu. Kwa wale ambao tumeishi zamani kidigo kabla ya uwApo wa mitandao hii, tunaweza kukubali kwamba huko nyuma mambo mengi yalikuwa magumu katika utendaji wake japo pia kulikuwa na faida za kutokuwapo kwa mitandao hii.

Faida mojawapo ni juu ya kulinda utamaduni mzuri katika jamii zetu. Hatukuwa tunahusiana sana hasa na utamaduni wa kigeni lakini leo mwingiliano umekuwa mkubwa sana kiasi cha kushindwa kulinda utamaduni wetu.

Vilevile katika suala zima la maadili, kwa sasa kunaonekana uwapo wa mmomonyoko wa maadili kwa kiasi kikubwa. Yaani maadili yamemomonyolewa kutoka kwenye misingi mikuu na haya yamefanyika kimkakati au kwa bahati mbaya. Yako mambo hayakuwa utamaduni wetu, lakini kwa sasa yanataka kufanywa kama ya kawaida na yanapigiwa debe na wale wanaoyaamini kama utamaduni wao. Hii yote ni kutokanana na utandawazi ambao kimsingi hatuwezi kuuepuka kwa sababu dunia imeshafanywa kijiji badala yake kuwa watumiaji wazuri.

Upande wa pili, mitandao hii imerahisisha mambo mengi yakiwapo mawasiliano, maarifa mbalimbali ya kijinga na ya maana, upatikanaji wa taarifa kwa haraka, mfano zamani kuwasiliana na mtu aliyeko mkoani au nje ya nchi lilikuwa jambo gumu sana lakini sasa tunaweza kufanya vikao vya kimataifa tukiwa majumbani mwetu.

Pamoja na mafanikio hayo, kumeibuka jambo baya la matumizi ya mitandao yasiyokuwa na kiasi, yaani matumizi ya muda mrefu kwa baadhi ya watu ambalo ndilo kundi kubwa. Watu tunashinda na kulala mitandaoni huku tukidhani tumelala majumbani. Baadhi ya shughuli zinakwama au kufanyika chini ya viwango kutokana na kutumia muda mrefu sana mitandao hasa kundi la vijana. Ni jambo linaloonekana la kawaida lakini nafikiri tumefika pabaya sana.

Ukitaka kujua hili, ingia kwenye daladala au kwenye chombo chochote cha usafiri. Utaona kila mtu ameshika simu yake mkononi akiwa mtandaoni. Watu wako kiti moja lakini hawazungumzi wala kusalimiana. Unachoweza kuona tu ni kila mtu anajichekesha akiwa anafuatilia jambo fulani mtandaoni.

Yale mazungumzo ya ana kwa ana yameuawa kifo cha kawaida kabisa na hii ni mpaka nyumbani mwetu, siku hizi anakuja mgeni anakaribishwa kisha kila mmoja anashika simu yake na kuanza kujichekesha kama mtu aliyepungua mahala fulani. Wakati mwigine tunapata wageni kutoka vijijini mpaka wanajisikia vibaya na kujuta kututembelea, maana unakuta familia nzima kuanzia watoto mpaka wazazi wako mtandaoni, watoto wakiwa kwenye magemu na wazazi wakiwa kwenye tikitoku, fesibuku, twita, makundi ya wasapu na kadhalika. Huu ndio unaitwa uraibu wa kimtandao.

Kwa haraka haraka, tunadhani haya ndiyo maendeleo lakini kuna athari kubwa sana za kijamii. Hata maandiko matakatifu yamesema kuwa na kiasi kwa kila jambo. Tunapokosa kiasi tunaathirika moja kwa moja. Wengine wanaenda mbali zaidi wamefika mahali pa kujibadilisha mpaka rangi zao za ngozi ili wafanane na wale wanaowatazama kila wakati mitandaoni. Unakuta binti wa miaka 16 amejikoboa ili mradi tu apige picha aonekane mzungu mweusi. Akifikisha miaka 40 atakuwa anafananaje?

Watoto wako kwenye hatari zaidi na hapa niwaase kinamama. Simu za kinamama zimetumiwa sana na watoto wadogo kama kinga ya kuzuia wasilie kama ambavyo watani zangu kule Iringa, walivyokuwa wanatumia kilevi aina ya ulanzi kuwatuliza watoto walipokuwa katika shughuli hasa za kilimo.

Matokeo yake, watoto wengi wanapokuwa watu wazima wanaingia kwenye ulevi wa pombe ndivyo itakavyotokea kwa watoto wetu. Mtoto kama anatakiwa kunyamaza anyamaze bila kutumia kitu kingine, tunadhani kwamba kwa kuwapatia simu tunaonyesha upendo wa hali ya juu mnatengeneza matatizo makubwa bila kujua.

Utasikia baadhi ya wazazi wanasema ohoo watoto wapewe tu maana ni vigumu kuzuia! Malezi gani hayo, tunataka kila anachokitaka mtoto tumpatie? Mbona hatuwapi sumu za panya maana yake tunafahamu wazi kuwa zinaua, kwa nini tusione matumizi ya simu katika umri mdogo ni hatari kama sumu ya panya?

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Bi harusi aliyemkana mchumba siku ya ndoa*



Na Adam Fungamwango

DUNIA hii ina mambo mengi ya ajabu yatakayokuacha mdomo wazi. Kuna mambo yanafanyika wakati mwingine unaweza kujiuliza kama ni kweli au ndoto. Binadamu wanafanya mambo ambayo wala huelewi walikuwa wanafikiria nini.

Utakuta baadhi ya wanaume wenye wake wa watoto, anaikimbia familia yake na kwenda kuishi kwa kimada, wakiacha wanateseka.

Baadhi ya wanawake, wanawakimbia waume zao, tena wakati mwingine wakibeba kila kitu ndani, kwa ajili ya kushawishiwa tu na mwanaume mwingine amkimbie mumewe, akidai atamuoa yeye baadaye.

Yote tisa, kuna wanaokimbiana hata siku ya harusi, kufunga ndoa au hata siku chache kabla ya hapo.

Nakumbuka mkasa mmoja, jamaa alikwenda kuoa maeneo ya Kibaha, akatoka na ndugu zake, Dar es Salaam, lakini walipofika huko hawakumkuta bi harusi.

Kina mama waliokuwa naye chumbani, walidai alitoroka muda machache tu kabla ya msafara wa bwana harusi kufika, na hawajui alikokwenda.

Alikuwa tayari ameshatoka saluni kupambwa, ina maana alikuwa tayari kwa kuolewa, lakini haikujulikana alipatwa na nini dakika chache kabla ya hapo. Wengine wakahusisha na imani za kishirikina.

Ilikuwa aibu kwa pande zote mbili. Upande wa bwana harusi ambaye alitoka na huyo zake, Dar, sasa atarejea bila mke. Ndugu wa bi harusi nao walipata aibu na kuonekana kama matapeli. Kila kilichofanywa, hakikuweza kuondoa ukweli kuwa bi harusi alikuwa ametoweka.

Mwaka mmoja baadaye, bi harusi alirejea na kila kitu kikajulikana. Kumbe alitokea kwa bwana jijini Dar es Salaam kabla ya kuwa na aliyetaka kumuoa, alikuwa na huyo jamaa, lakini hakuwa na pesa ya kuridhisha, hivyo akaamua aolewe na mtu mwingine.

Wakati sherehe imeshapangwa, akapigiwa simu na bwana'ake huyo wa Dar kuwa amepiga pesa nyingi ambazo zingemwezesha kuishi maisha mazuri, hivyo akamtaka aende. Na kwa kuthibitisha, akamtumia shilingi laki moja na nusu kwenye simu yake. Hiyo ilimtoa kichaa bi harusi, akaamua kufanya aliyoyafanya.

Ni kweli ilikuwa hivyo. Lakini baada ya muda jamaa yake alikamatwa, kwa sababu pesa zile zilikuwa za wizi. Bi harusi alirudi nyumbani na kuomba akabembelezewe na aliyetaka kumuoa. Sijui waliishia vipi. Sasa kuna huyu, ambaye ameimbwa na bendi ya Vijana Jazz Band.

Yeye amemkana mchumba wake laivu mbele ya kasisi aliyekuwa anawafungisha ndoa. Pamoja na kuulizwa mara tatu kama anakubali kuwa mumewe, bi harusi akakataa. Mpaka leo haijajulikana tatizo lilikuwa nini? Si angekataa tangu mwanzo? Ilikuwa na haja gani kujiandaa, kwenda saluni, kuvaa shela, na kwenda kukataa mbele ya mashahidi? Je alilazimishwa?

Mwanamke sasa aliwapa watu la kusema mitaani na kumtoa aibu mchumba wake mbele ya ndugu, jamaa, wazazi na rafiki zake.

Katika wimbo huu, uliorekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1990, utunzi wake, Jerry Nashon 'Dudumizi', mwanamume ndiye anamlalamikia aliyetaka kuwa mkewe kwa jinsi alivyomuaibisha siku ile.

"Aibu, aibu, aibu umenipa, umenipa aaa mamaaa.Aibu, aibu, aibu umenipa, umenipa aaa mamaaa. Ulinikataa, siku ya harusi, mbele ya kasisi, bibi, ukanikimbia, mbele ya wazazi na rafiki zangu, Tereza aaa.

Nasema, kwa heri kwa uchungu, moyo wangu, unawaka aaa Tereza. Nasema, kwa heri kwa uchungu, moyo wangu, unawaka aaa Tereza.

Umeniambia, unaye mwingine wa kukuliwaza na kukupumbaza bibi, hiyo pete yangu, usiirudishe, ni uthibitisho wa penzi langu kwako."

Pamoja na yote, jamaa anamwambia pete aliyomvalisha abaki nayo kwa sababu ni uthibitisho kuwa bado anaendelea kumpenda.

"Najiuliza kila mara na kujuta moyoni, ni penzi gani analokupa huyooo, ni dawa gani aliyekunywesha, ukachanganyikiwa na kuisahau sura yangu, siku ya harusi.

Tereza, penzi gani analokupa wewe Tereza, nami pia nitajifunza Tereza, akikupa busu la shavu mpenzi Tereza, nitakupa la kinywani ooo Tereza, bibi iii.

Tereza, chakula gani anachokupa wewe Tereza, nami pia nitakupa nitaweza, akikupa wali na sombe mpenzi Tereza, nitakupa wali na pono, Tereza mama, bibi iii.

Tereza, penzi gani analokupa wewe kijana, nami pia nitakupa, Tereza, kama pochi nami ninalo mpenzi Tereza, sema nitakupatia, Tereza, bibii." Jamaa anaendelea kulalamika, akidhani kabla kuna vitu anazidiwa na mwanaume mwingine.

"Najiuliza kila mara na kujuta moyoni, ni penzi gani analokupa huyooo, ni dawa gani aliyekunywesha, ukachanganyikiwa na kuisahau sura yangu, siku ya harusi.

Bibi iii, ni nguo hujavaa wewe eee, kinywaji gani hujakunywa mama aa, basi sema raha ipi unataka ili nielewe, niiponye roho yangu uuu.

Bibi iii, ni mji gani hujafika wewe eee, hoteli gani hujalala mama, basi sema raha ipi unataka, ili nielewe, niiponye roho yangu uuu."

Jamaa anaonekana bado anataka apewe nafasi nyingine, kwani anamuuliza nini anahitaji, nguo, kinywaji, au apelekwe mji gani, au hoteli nzuri ili amkubalie, waandae tena ndoa. Hii ndiyo dunia yenye maajabu, utaona mengi, yatakukuta mengi, utayapata mengi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam.
Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia.
Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa.
Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi.
Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Damu ya Mariamu-13

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)




Heri hakubakisha chochote. Alimwambia kila kitu kama vile mtuhumiwa anavyomuweka wazi wakili wake ili ajue wapi kwa kuanzia kumtetea hadi mwisho wa kesi. Wakili hatakiwi kudanyangwa. Kudanganywa kunaweza kumfanya akashindwa mbinu za kumtetea mteja wake. Unapomwambia ukweli hata kama umetenda kosa, ana mbinu za kiufundi, mbali na elimu yake jinsi ya kumuondoa mteja wake kwenye shtaka.

"Duh! Pole sana kijana. Hiyo ndiyo dunia. Haya mambo yapo kwenye maisha. Sasa unaanza kukomaa kijana. Umeanza kuwa mwanaume." Akauongea mzee Raia huku akitabasamu.

Hali hiyo limshangaza Heri. Wakati yeye akiwa na hofu kubwa, lakini mzee Raia alionekana kama kulichukulia jambo hilo poa.

"Hivi huyu mzee hajamuona Nuru hali yake nini?" Akauliza kimoyomoyo.

"Sawa, hebu twende nyumbani kwako tukaangalie hiyo hali, halafu tuone tunafanyaje."

Kitendo cha mzee Raia kukubali kirahisi hivyo, licha ya kile alichomueleza kikionekana kuwa cha kutisha, kilimfariji Heri.

Kwake ilionekana ni kama vile nusu nzima ya tatizo zimeshatatulika. Na kwa jinsi alivyoona mzee alivyolichukulia. Hakuonekana kupaniki, kwake ilionekana ni uamuzi sahihi alioufanya kwenda kumuita mzee huyo.

Waliondoka taratibu kama mzee Raia alivyomwambia, Heri kuwa hakuna haja na kutembea haraka haraka kwani mwendo huo ungewavutia watu na kutaka kujua kuna nini.

Heri alitangulia kufungua geti na kwenda moja kwa moja hadi kwenye mlango wa chumba chake na kufungua taratibu. Hakuingia moja kwa moja, badala yake akachungulia kufahamu aliyemuacha kwa sasa yupo kwenye hali gani.

Hali ilionekana kuwa mbaya zaidi. Nuru alikuwa akitetemeka mara dufu kuliko ilivyokuwa awali. Alikuwa akitoa sauti kubwa ya muungurumo ambao ulimtisha Heri na kushindwa kupiga hatua yoyote kuingia ndani.

Ilibidi mzee Raia naye asogee karibu na Heri, naye akachungulia ili kuona ni kitu gani kinachoendelea.

Hakuna kilichoongezeka zaidi ya kile kile ambacho aliambiwa na Heri, awali.

"Ahaa, kumbe! Sasa sikiliza kijana! Usiogope. Tuingie ndani." Mzee hakuongea na maneno, bali kwa vitendo. Yeye mwenyewe aliingia chumbani na kumuacha Heri nje akionekana kama mwiga hivi.

> **"Enhee, tuambie tatizo lako nini?" Akauliza mzee Raia. "Kiti amekuja kwa rijali, mimi sitaki hiki kitu, nimekuja kutoa onyo kwa kiti na mwenzake, kama wakifanya kitendo chochote cha mahusiano nitawakatakata na kuwanywa damu zao wote wawili."**

Mzee Raia alipoingia ndani, hakwenda moja kwa moja kwa msichana Nuru, bali alionekana kuzunguka chumba kizima akionekana kama mtu anayechunguza hiki na kile.

Baadaye alipoonekana kuridhika na uchunguzi wake, akageuka nyuma na kumkuta Heri akiwa naye anaingia kwa hatua fupi fupi za wasiwasi.

"Sasa unasikia kijana, njoo tumbebe tumtoe nje hapo apigwe na upepo." Heri alimshangaaa mzee Raia, kwani alitegemea kusikia tumbebe na kumpeleka hospitali.

Akatii amri, yeye alimnyanyua juu, na mzee Raia akamshika miguuni, wakamtoa nje ya chumba na kumuweka chini.

Kwa bahati nzuri ni kwamba sehemu hiyo ilikuwa ni uani, kukizibwa na ukuta wa matofali, pamoja na mlango mkubwa.

Kwa maana hiyo hakuna yeyote aliyeliona lile tukio, tofauti na ingekuwa zile nyumba ambazo hazina ua. Ni lazima angetolewa barazani ambako watu wangekuwa wanapita na kukutana na tukio lile, ambalo lazima lingejaza umati.

Tayari ilishatimu saa moja usiku, na wapangaji wenzake wa vyumba vya uani walikuwa bado hawajafika.

Bahati nzuri nyingine ni kwamba nyumba hiyo ilijengwa kwa staili ya watu wanaishi kwenye nyumba kubwa hawachanganyiki, au kuja kwa wale wa vyumba vya uani bila kupitia kwenye mlango mkubwa wanaouita geti.

Wale wa nyumba kubwa nao wana mlango wao wa barazani, na wakitaka kwenda vyumba uani ni lazima wazunguke na kwenda kuingia kwenye kigeti.

Yote hayo yalisababisha tukio lile libaki kuonwa na watu hao tu wawili.

"Enhee wewe ni nani?" Mzee Raia aliuliza, swali ambalo lilimshtua Heri ambaye hakujua nani anaulizwa, yeye au?

Ghafla Nuru alipiga kelele kali ambayo, ilimsthua zaidi Heri kuliko mzee Raia, halafu ikasikika sauti ambayo ilitoka kinywani mwake.

"Mimi ni jini Anzura." Sauti ikatoka mdomoni kwa Nuru ambayo ilimshangaza Heri, kwani si ya Nuru aliyemzoea.

"Enhee, tuambie tatizo lako nini?" Akauliza mzee Raia. "Kiti amekuja kwa rijali, mimi sitaki hiki kitu, nimekuja kutoa onyo kwa kiti na mwenzake, kama wakifanya kitendo chochote cha mahusiano nitawakatakata na kuwanywa damu zao wote wawili."

"Sawa tumekusikia Anzura, sasa tunatakiwa kufanya nini?" "Kiti aondoke mara moja kwa rijali, la sivyo nikirudi tena sitokuwa na huruma yoyote, huyu ni wangu hawezi kuolewa."

Maneno yaliyokuwa yakizungumzwa na sauti ya ajabu iliyotoka kinywani mwa Nuru ilimtisha Heri.

Ile kuambiwa kuwa kama wangeshiriki mapenzi, basi wangekatwakatwa na damu yao kuwa kisusio, kulimfanya kidogo atimue mbio.

Lakini utulivu, umakini aliokuwa nao mzee Raia ndiyo uliomfanya asite kufanya hivyo, akiona yeye ndiye mwokozi wake, kwani anaonekana kusikilizana na amri ya sauti ile.

"Tumekusikia, na tutatekeleza, tunakuomba uondoke urudi kwako, tunatekeleza maagizo yote."

Kikatokea kicheko kikali, ambacho pamoja na kuwa kilikuwa cha furaha, lakini kilisikika kwa namna ya kutisha, halafu Nuru akaanza kujinyoosha na nguvu ile aliyoonekana nayo mwanzo ilianza kumuishia. Kwa muda mfupi ikarejea ile ya kike, na akaonekana kupatwa na usingizi.

"Sasa muache alale hapa apigwe na upepo." Mzee Raia akamwambia Heri, ambaye wakati huo alikuwa amesimama, lakini mwili mzima ukitetemeka kwa hofu kwa kile alichokiona na kukisikia.

Dakika tano zilipita, ndipo Nuru alipoonekana kupatwa na fahamu. Akainuka. Akawatazama watu wawili waliokuwa mbele yake. Akashangaa kidogo, lakini akatabasamu, huku akionekana na aibu.

"Pole mama." Mzee Raia alimpa mkono. Heri hakuonekana kusema chochote. Alikuwa akimtazama Nuru kwa huruma, iliyochanganyikana na woga pia.

Alikuwa akiwaza kuwa kumbe kitendo chochote ambacho angefanya na Nuru ilikuwa apate matatizo makubwa ambayo yangepoteza maisha ya wote wawili.


Nuru akaitikia kwa kichwa. "Endelea kupumzika, ndani mle nimeona kama kuna mswala hivi, lete ili bibie akalie apumzike, halafu nitazungumza naye baadaye."

Baada ya kuuleta na kumweka apumzike hapo, akamwambia aende dukani kumnunulia chupa ya maji, kwani katika hali aliyokuwa nayo, ni wazi amepoteza maji mengi.

Alichukua dakika mbili mpaka kurejea kwani duka halikuwa mbali sana na hapo.

"Sasa rafiki yangu, njoo ndani nikwambie kitu gani kimesababisha hadi binti huyu amekuwa katika hali hii, na kiumbe gani kilikuwa kinazungumza kwa sauti iliyotoka kwenye kinywa chake."

**Itaendelea Jumapili**



# TYLA AWABURUZA WANIGERIA BET 2024

MWANAMUZIKI wa Afrika Kusini Tyla, amewapiga kikumbo wasanii wa Nigeria baada ya jina lake kuchomoza vyema na kuteuliwa katika vipengene vinne katika tuzo za BET 2024.

Tyla amewapiku mastaa wa Nigeria Ayra Starr, Burna Boy, Tems, Asake, Seyi Vybez, Davido na Lojay.

Ayra Starr ameshika nafasi ya pili kwa wasanii wa Kiafrika kwa kuteuliwa mara tatu, akifuatiwa kwa karibu na Burna Boy na Tems ambao wanawania tuzo katika vipengele viwili.

## BAMBO AMNG'ANG'ANIA DIAMOND

MSANII wa vichekesho, Bambo, amezidi kulalamika kwa kudai kwamba mwanamuziki Diamond Platnumz, anahusika kwa namna moja kushushwa kwenye jukwaa wakati akiburudisha.

Bambo amesema kwamba tukio hilo limemfanya kumchukia kwani inaonyesha jinsi Sanaa ilivyojaa chuki na kukatishana tamaa.

"Tulipanda jukwaani na Mtanga lakini tukiwa tunacheza ghafla alikuja baunsa wa Diamond na kuja kutuondoa kwa nguvu, kitu hiki kimeniumiza sana," amesema Bambo.



## ZISIKUPITE

### BRUNO NA BAYERN

BAYERN Munich ina mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United, Bruno Fernandes msimu huu wa majira ya joto na inaamini kuwa inaweza kumpata mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 29. ***(Independent)***

### TUCHEL SASA KUBAKI

WACHEZAJI wa Bayern Munich akiwemo mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30, wanataka kocha Thomas Tuchel kubadili uamuzi wake wa kuondoka katika klabu hiyo ya Bundesliga mwishoni mwa msimu huu. ***(Abendzeitung)***

### BRANTHWAITE NA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kutoa pauni milioni 55 kumnunua beki wa Everton na England mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite. ***(Daily Mail)***.

### FRIMPONG KUONDOKA

MLINZI wa Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 23, anaelekea kuondoka Beyer Leverkusen msimu huu wa majira ya joto huku Real Madrid, Manchester City, Arsenal na Manchester United zikiwa na nia ya kunufaika na kipengele cha pauni milioni 35 katika mkataba wake. ***(Bild)***

### GUIMARAES ANYATIWA

ARSENAL na Manchester City zimewasiliana na kiungo wa kati wa Newcastle United na Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26, kuhusu uwezekano wa uhamisho msimu huu a majira wa joto. ***(Caughtoffside)***

### FRANK ATAJWA MAN

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank ni miongoni mwa makocha wanaotarajiwa kujiunga na Manchester United endapo wataamua kumfuta kazi, Erik ten Hag. ***(Telegraph)***

### NAPOLI NA CONTE

NAPOLI itampa kocha wa zamani wa Chelsea na Tottenham Hotspur, Antonio Conte pauni milioni 5.6 kwa mwaka kuwa kocha wao ajaye lakini nia ya AC Milan ya kumnunua Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 54 imefifia. ***(Sport Italia)***

### EMERSON ASAKWA

AC Milan inamsaka beki wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 25 raia wa Brazil, Emerson Royal. ***(Fabrizio Romano)***

### ADARABIOYO AGOMBEWA

MANCHESTER United ipo kwenye mbio moja na Newcastle United kawania kumnunua beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Talksport)***

### THURAM KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL imepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Nice na Ufaransa, Khephren Thuram mwenye umri wa miaka 23 kwa pauni milioni 13 msimu huu. ***(Mirror)***

### HULSHOFF KUTEULIWA

KOCHA wa Feyenoord, Arne Slot anapanga kumfanya kocha wake msaidizi, Sipke Hulshoff kwenda nae Liverpool atakaporithi mikoba ya Jurgen Klopp. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JUVENTUS YAMTIMUA KOCHA ALLEGRI

**Kocha huyo amefukuzwa kazi siku chache baada ya kutwaa ubingwa wa Coppa Italia kwa kuwafunga....**

**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri amefukuzwa kazi na Juventus, klabu hiyo imetangaza, ikiwa ni siku chache baada ya kuifunga Atalanta na kubeba taji la Coppa Italia.

Juventus wamebakiza mechi mbili kabla ya Serie A kufikia mwisho msimu huu, lakini Allegri alipaswa kuzikosa kufuatia kufungiwa michezo miwili kutokana na tabia yake kwenye fainali Jumatano.

Allegri alipoteza utulivu katika dakika za lala salama alipokasirishwa na maamuzi, akavua koti lake na kupata kadi nyekundu kwa kumshangilia mwamuzi kwa kejeli Juventus ilipoilaza Atalanta 1-0.

Juventus walisema katika taarifa [redacted]

Pamoja na kusimamishwa, pia alipigwa faini ya dola 5,400 na bodi ya Serie A.

Vyombo vya habari vya Italia viliripoti kwamba Allegri pia alikuwa mkali dhidi ya waandishi wa habari baada ya mechi.

Shirikisho la soka la Italia linaangalia matukio wakati wa fainali.

"Tunaweza kuthibitisha kwamba uchunguzi juu ya tukio (ambalo) lilitokea wakati wa Fainali ya Coppa Italia, ambapo ... Allegri na Mkurugenzi wa gazeti la Tuttosport Guido Vaciago walihusika, ni kwa wakati ufaao kati ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa FIGC," FIGC ilisema katika taarifa Yake.

Mbali na Kombe la Italia, Juventus imekuwa na msimu wa kukatisha tamaa.

[redacted]

kushiriki mashindano ya Ulaya kutokana na kesi ya uwongo ya uhasibu.

Allegri alikuwa katika kibarua chake cha pili Juventus, baada ya kujiunga tena na klabu hiyo Julai 2021.

Alifanikiwa zaidi katika muhula wake wa kwanza na Bianconeri hao, akishinda mataji matano mfululizo ya Serie A kuanzia 2015 hadi '19.


Taji lake pekee tangu arejee ni Kombe la Italia aliloshinda wiki hii, ambayo imekuwa mechi yake ya mwisho akiwa na timu hiyo.

Juventus haikutangaza mara moja mbadala wa Allegri. Kumekuwa na tetesi kuwa klabu hiyo inataka kumwajiri Thiago Motta kutoka Bologna.

## HABARI MICHEZO

# MAN CITY NAFASI NYEUPE KUBEBA TAJI LA NNE MFULULIZO EPL LEO

**MANCHESTER, England**



PEP Guardiola amewaambia wachezaji wake wa Manchester City kwamba West Ham itafanya kila kitu kuwazuia kushinda taji la nne mfululizo la Ligi Kuu leo Jumapili.

City wanahitaji kuifunga West Ham kwenye Uwanja wa Etihad leo ili kutawazwa mabingwa.

West Ham hawana lolote kwenye mchezo huo na David Moyes, ambaye anaondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu, amesema "itakuwa vigumu kuwazuia vijana wa City kushinda taji."

Ingawa City imekuwa na hofu ya siku ya mwisho, ikihitaji mabao ya dakika za mwisho ili kurejea kutoka kwa kupoteza nafasi za kushinda dhidi ya QPR mwaka 2012 na Aston Villa mwaka 2022.

"Yeye (Moyes) atafanya kila kitu kutushinda," Guardiola aliwambia wanahabari juzi.

"Niko tayari kwa mchezo mgumu. Nataka kuweka akilini mwa wachezaji wanaoitazama Tottenham, jinsi walivyopigania kila mpira.

"Ilikuwa ni uchokozi wa ajabu na kujitolea kwa Spurs. Sikuwa na shaka juu ya hilo. Wachezaji 11 wa West Ham watakuwa tayari kutushinda. Hilo lilitokea Aston Villa wakiwa katika nafasi sawa na kucheza kwa misimu miwili iliyopita na najua ni nini kilifanyika.

Guardiola amekutana na Moyes mara 15 kama kocha na kupoteza mara moja pekee huku City wakiwa hawajafungwa katika mechi 16 zilizopita dhidi ya West Ham.

Ushindi wa leo utamfanya Guardiola kutwaa taji lake la sita la Ligi Kuu England na kuipa City nafasi nyingine katika historia kama timu ya kwanza ya Uingereza kushinda mataji manne ya Ligi mfululizo.

Arsenal walio katika nafasi ya pili wanaweza tu kutumaini kwamba City watapoteza pointi na watafaidika na kuwashinda Everton huko Emirates.

"Ukiuliza timu zote za Ligi Kuu mwanzoni mwa msimu ni nafasi gani itakuwa bora kwa mchezo wa mwisho wa msimu, tuko kwenye nafasi bora," Guardiola alisema.

"Hiyo ni hakika. Mchezo mmoja, hatima mikononi mwetu. Tunahitaji kushinda mchezo mmoja ili kuwa mabingwa. Kila timu ingependa kuwa katika nafasi yetu, hilo ni la uhakika.

"Lakini haitakuwa rahisi."

# Xavi atibua hali ya hewa Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

MUSTAKABALI wa Xavi Hernandez ndani ya Barcelona umeingia kwenye mtafaruku mpya baada ya kocha huyo kumkasirisha Rais na wajumbe wa bodi kutokana na maoni yake kuhusu hali ya kiuchumi ya klabu hiyo.

Maisha yake ya ukocha katika klabu aliyopata heshima kubwa akiwa kama mchezaji yapo kwenye hali tete.

Baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Almeria, Xavi alisema:

"Kila shabiki wa Barca lazima aelewe kwamba hali ya uchumi ni mbaya na kuna kazi kubwa ya kushindana kiuchumi.

"Lazima wajue hali yetu ya sasa si sawa na miaka 25 iliyopita ambapo kocha alikuwa akisema 'Namtaka huyu, huyu, na huyu, anampata'. Kwasasa haiko hivyo tena.

"Ninaelewa hali iko hivyo na tunapaswa kuzoea, haimaanishi kwamba hatutashindana uwanjani lakini tunahitaji utulivu mkubwa.

"Nasema hivi kwasababu nimekifikiria, hali yetu ya uchumi si nzuri na sote tunafanya kazi vizuri sana kuboresha hali hiyo. Tutapambana kupata mataji, hakuna kinachobadilika.'

Wakurugenzi wa Barcelona wamekasirishwa na kitendo cha Xavi kusema maneno hayo hadharani kuhusu hali yao ya kifedha ndani ya klabu hiyo.

Lakini pia Rais Joan Laporta alikasirishwa na maneno hayo.

Fabrizio Romano ameripoti kuwa mazungumzo ya pande zote mbili yanaendelea na Rafael Márquez raia wa Mexico ambaye anaifundisha Barcelona B anatajwa zaidi kurithi mikoba ya Xavi.

Mbali na hilo, Imeelezwa kuwa uhusiano wa bwana mdogo Vitor Roque na Xavi Hernandez unajadiliwa ambapo hivi karibuni wakala wa mchezaji huyo amekuwa akilalamika kuhusu mustakabali wa mchezaji wake ndani ya timu hiyo huku ikielezwa kuwa Xavi hana mpango na mchezaji huyo na hazungumzi nae.



## Kane azusha hofu kwenda Euro

**MUNICH, Ujerumani**

NAHODHA wa England, Harry Kane amezusha hofu baada ya kupata jeraha la mgongo ikiwa ni chini ya mwezi mmoja kabla ya michuano ya Euro.

Kane alilazimika kukaa nje kwenye mechi ya mwisho ya Bayern ya Bundesliga dhidi ya Wolfsburg Mei 12, na hakuwepo kwenye safari yao dhidi ya Hoffenheim jana.

Kocha wa Bayern, Thomas Tuchel alisema Kane alikuwa akipambana na jeraha hilo katika maandalizi ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya Bayern dhidi ya Real Madrid mnamo Mei 8 lakini alicheza na maumivu.

"Harry anapokea matibabu kutoka kwa daktari wake binafsi," alisema Tuchel.

"Tayari alikuwa kwenye kikomo huko Madrid. Alikuwa na kizuizi kamili mgongoni mwake, imekuwa mbaya zaidi na inamsumbua katika harakati za kila siku."

Kane amekuwa na msimu mzuri sana akiwa na Bayern, akimaliza kampeni yake ya kwanza ya Bundesliga akiwa na mabao 36, ikiwa ni pamoja na hat trick nne.

Ana mabao 44 kwa jumla wakati wa kuleta mchango wake kwenye Ligi ya Mabingwa, huku pia akiwa na pasi za mabao 12 kwenye mashindano yote.

Habari za kuumia kwake zimeleta wasiwasi kwa timu ya England wakati wanajiandaa kwa Euro 2024, ambapo watakuwa moja ya timu inayopewa nafasi kubwa ya kushinda ubingwa huo hilo.

Kane anatazamiwa kuwa nahodha wa timu hiyo msimu huu wa majiraya joto na atakuwa mmoja wa watu muhimu wakati wanatazamia kushinda kombe kubwa la kwanza la wanaume tangu 1966.

Kocha wa England, Gareth Southgate atataja kikosi chake kwa ajili ya michuano hiyo kwenye Uwanja wa St. George's Park siku ya Jumanne, huku Kane akiwa bado anatarajiwa kujumuishwa.

Ratiba ya England inawakutanisha wakicheza mechi mbili za kirafiki kabla ya michuano hiyo. Ya kwanza dhidi ya Bosnia na Herzegovina Juni 3 ikifuatiwa na Iceland Juni 7.

England itaanza kampeni yake ya Euro 2024 dhidi ya Serbia Juni 16.

HABARI MICHEZO

# KIZUMBI AWASHUKURU MASHABIKI YANGA

**Na Saada Akida**

LICHA ya uongozi wa klabu ya Yanga kutoweka wazi usajili wa winga wa kulia wa TP Mazembe raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Phillipe Kizumbi, mchezaji huyo amejitokeza na kuwashukuru mashabiki wa klabu hiyo kwa kumkaribisha na kumfanya aongeze marafiki wengi katika mitandao yake ya kijamii.

Inaelezwa Yanga wameshamalizana na mchezaji huyo na msimu ujao atacheza Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na mabingwa hao.

Nyota huyo juzi aliposti video fupi akiwa amevaa jezi ya Yanga, akiwashukuru mashabiki wa klabu hiyo kuwa sehemu ya familia ya Mabingwa hao.

Mchezaji huyo alisema anafurahi kuona mashabiki wa Yanga wamejitokeza kwa wingi kuungana naye na kumkaribisha kwenye timu yao na kuendelea kuongeza marafiki.

"Nawapenda Yanga wote na nashukuru kwa kuonyesha upendo huu mkubwa, msisahau kunifuatilia najua mnaweza kufanya hivyo jamani, naipenda Tanzania tutaonana hivi karibuni," alisema nyota huyo kwenye mtandao wake wa kijamii.

Kizumbi alisema anaimani ipo siku atakuja Tanzania lakini hakuweka wazi juu ya timu gani atakuja kucheza na kuwataka mashabiki wake kuvumilia kwa sababu lolote linaweza kutokea katika masuala ya usajili.

Kizumbi ambaye ni mchezaji halali wa TP Mazembe ambayo imeingia makubaliano na Yanga ya kubadilishana wachezaji.

Inaelezwa, Kizumbi atatu Jangwani na mshambuliaji Kennedy Musonda atajiunga na TP Mazembe katika muda wake wa mwaka mmoja uliobaki kwenye mkataba wake.

Mbali na mchezaji huyo tayari Yanga ipo katika mazungumzo na kipa wa Tanzania Prisons, Yona Amos kuchukuwa nafasi ya Metacha Mnata ambaye klabu hiyo ina mpango wa kuachana naye mwishoni mwa msimu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), akifanya mazoezi na washiriki wa mbio za 'Pugu Half Marathon' zilizofanyika Pugu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Watu 7000 washiriki Pugu Marathon

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa jana aliwaongoza watu 700 kushiriki mbio za hisani za Pugu Marathon zenye lengo la kuwasaidia watu wenye uhitaji.

Mbio hizo zilifanyika jana Pugu, jijini Dar es salaam na kuhudhuriwa pia na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo.

Waziri Mkuu aliwapongeza waandaaji wa mbizo hizo na kuwaomba ziwe endelevu.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati ya Pugu Marathon, Richard Sillo alisema mbio hizo zinafanyika kwa mara ya pili mwaka huu ambapo lengo ni kuhakikisha wanasaidia wenye uhitaji na kuchangia damu.

Alisema mbio hizo zina malengo ya kukusanya fedha za kukarabati miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Pugu, ikiwemo maktaba, nyumba aliyowahi kuishi Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

"Tumeandaa mbio hizi ambazo zinafanyika mara ya pili mwaka huu, lengo kubwa ni kuchangisha fedha za kusaidia wenye uhitaji, kukarabati maktaba ya shule na nyumba ya Nyerere, lakini kuifanya Pugu kuwa sehemu ya kimataifa katika mambo ya utalii," alisema Sillo.

Alisema kwa mwaka huu jumla ya wakimbiaji 7,000 walishiriki mbio hizo na washindi walijipatia zawadi mbalimbali.

## Yanga, Ihefu mechi ya kisasi

INATOKA UK. 24

Mexime.

Katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza jana uliochezwa kwenye uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Azam FC walifanikiwa kutinga hatua ya fainali baada ya kuibuka na ushindi wa bao 3-0.

Katika mchezo huo, Coastal Union licha ya kuonyesha upinzani mkubwa walishindwa kuzima ndoto za Azam za kutinga fainali ya pili ya michuano hiyo inayodhaminiwa na benki ya CRDB.

Azam sasa wanasubiri mshindi wa mchezo wa leo kucheza nao fainali itakayofanyika Juni 2 mkoani Manyara.

Mabao ya Azam jana yalifungwa na Abdul Suleiman 'Sopu' aliyefunga mabaomawili katika kila kipindi na Feisal Salum 'Fei Toto' aliyefunga kipindi cha pili.

## Mgunda: Mapambano yanaendelea

INATOKA UK. 24

nimefanya vizuri, mashabiki wamenipokea vizuri," alisema golikipa huyo ambaye alipata nafasi hiyo baada ya makipa wengine watatu, Ayoub Lakred, Aishi Manula, na Ally Salim kutokuwepo kwa sababu mbalimbali.

Matokeo ya juzi yanaifanya Simba kufikisha pointi 60, sawa na Azam FC, zote zikiwa zimecheza michezo 27, lakini Wanalambalamba wanashika nafasi ya pili kwa kuwa na uwiano mzuri wamagoli ya kufunga na kufungwa.

Azam imefunga mabao 54, imefungwa mabao 20 huku Simba wakiwa wamefunga mabao 52 na kufungwa mabao 24.

Timu zote mbili zimebakisha mechi tatu na yoyote itakayomaliza nafasi ya pili itaungana na mabingwa Yanga, kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Francis Baraza, alisema kosa walilofanya ni kuruhusu bao mapema.

"Naweza nikasema Simba walipata bao lao mapema na wakaweza kulizua hadi mwisho, ndiyo mchezo. Kusema kweli Ligi ni ngumu na kila mtu ameona, iwe nyumbani au ugenini, kila unayecheza naye anakaza, sasa hesabu zangu zipo kwa Yanga, Ihefu, na Mashujaa, mechi zote ni kama fainali", alisema Baraza

Dodoma Jiji ipo nafasi ya 11, ikiwa na pointi 30 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

Michezo
Jumapili Mei 19, 2024
Nipashe



Xavi atibua hali ya hewa Barcelona UKURASA 22

# Mgunda: Mapambano yanaendelea

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amesema mapambano ya kuitafuta nafasi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara yanaendelea licha ya ugumu na changamoto nyingi.

Akizungumza jana mara baada ya mechi ya raundi ya 27 ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji mchezo uliochezwa juzi kwenye uwanja wa Jamhuri Dodoma na Simba kuibuka na ushindi wa bao 1-0, Mgunda alisema wataendelea kupambana kadri itakavyowezekana kuweza kupata nafasi hiyo ili wacheze Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Alisema ni utamaduni wa Simba ni kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na watapambana kuisaka tiketi ya kushiriki michuano hiyo.

"Mechi ilikuwa gumu kutokana na mahitaji ya kila timu, dakika ya kwanza hadi ya 90, pamoja na yote tunamshukuru Mungu, tumepata pointi tatu katika mchezo mgumu, katika uwanja mgumu, umemalizika tunajipanga na mechi nyingine, lengo letuni kuhakikisha tunapata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Mgunda..

"Timu yetu tatizo ni lile lile tunatengeneza nafasi, kuzitumia imekuwa changamoto, tutajitahidi tuzitumie, lakini wakati mwingine inakuwa ngumu kwa sababu hata wapinzani wetu wanapambana ili kutuzuia, mchezo wa mpira wa miguu ndivyo ulivyo, vinginevyo tungefungana mabao mia kwa mia," alisema kocha huyo wa zamani wa Coastal Union.

Kwa upande wa kipa, Hussein Abel, aliyedaka mechi yake ya kwanza msimu huu, akikaa dakika 90 langoni bila kuruhusu bao alisema yeye yuko tayari wakati wowote ule kusimama langoni kwa sababu ameshaandaliwa kupambana.

"Mimi niko tayari muda wowote kwa sababu nimeandaliwa kupambana, nashukuru Mungu nimepewa nafasi, nimeaminiwa,

INAENDELEA UK 23



# YANGA, IHEFU MECHI YA KISASI

- Gamondi ataka shughuli iishe ndani ya dakika 90, Azam watangulia fainali...

**Na Faustine Feliciane**

YANGA leo inashuka kwenye uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini kusaka tiketi ya kucheza fainali ya Kombe la FA itakapoumana na Ihefu kwenye mchezo wa nusu fainali.

Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi akizungumzia mchezo huo wa leo, alisema wamejiandaa vizuri lakini angependa vijana wake wamalize kazi ndani ya dakika 90.

Gamondi alisema hatarajii mchezo mwepesi na hivyo wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi utakaowapeleka hatua ya fainali watakayocheza na Azam ambao jana walifanikiwa kutinga hatua hiyo kwa kuifunga Coastal Union.

Gamondi, alisema malengo yao msimu huu ni kutwaa makombe yote ya ndani na wanahitaji ushindi leo kuweka hai malengo yao ya kuchukua vikombe vyote.

"Tulikuwa na melngo yetu tangu kuanza kwa msimu huu, asilimia kubwa tumefanikiwa, tumecheza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na sisi malengo yetu yalikuwa kufika hatua ya makundi, tumetwaa ubingwa wa Ligi Kuu, sasa kazi imebaki kwenye michuano hii ya kombe la FA, tunalitaka," alisema Gamondi.

Alisema wanatarajia upinzani kutoka kwa Ihefu lakini amewataka wachezaji wake wapambane kuhakikish wanapata alama tatu na kwenda fainali ya michuano hiyo.

Kwa upande wake, Kocha wa Ihefu, Mecky Mexime, alisema vijana wake wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo wa nusu fainali.

Alisema wanafahamu ugumu wa wapinzani wao lakini wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo wa nusu fainali.

"Tunawaheshimu yanga kwa ubora wao, wametwaa ubingwa wa Ligi Kuu, lakini na sisi tumejiandaa kuhakikisha tunapata ushindi, litakuwa jambo zuri kama tutaingia fainali, tumejipanga kukabiliana nao," alisema

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >